# Kufanywa Wana Wenye Mamlaka #4

Jeffersonville, Indiana, USA

Mei 22, 1960

1 Ndugu Neville, nahabari za alasiri, jioni, ndiyo namaanisha, kwa marafiki wetu wa thamani, tuna furaha kurudi hapa kanisani usiku wa leo. Kuna joto kidogo, na kwa hiyo tutajaribu kuharakisha upesi iwezekanavyo, tuingie moja kwa moja kwenye Ujumbe. Kwanza, tuna matangazo ya kufanya, na—na haja maalum ya maombi. Nilipata barua zenu huko nyuma,zilizotolewa, na kwa ajili ya yule dada anayejisikia ana uvimbe kwenye ubongo. Na kulikuwako na mwingine huko Louisville; na ndugu wa mhudumu mwingine, baba yake ana ugonjwa wa mshtuko wa moyo; na kuna watu wengi, watu wengi wagonjwa ulimwenguni leo. Wengi wanatupigia simu nasi bila shaka tunawaombea kwa mioyo yetu yote, kwamba Mungu atatusaidia.

2 Kwa kawaida karibu asilimia tisini na tano ya huduma yangu daima ni hilo, kuwaombea wagonjwa, unaona, lakini ni-nilipata kwa namna fulani ninii—kwa namna fulani nilipata wazo fulani la jambo hilo … Bado ningali nawaombea wagonjwa, sasa, kumbukeni jambo hilo. Hilo linaambata moja kwa moja nayo. Lakini, loo, kama tunaweza kuliweka ka—kanisa mahali pake, basi, likae katika utaratibu ili tuweze kwenda kazini, unaona. Inatupasa kujiandaa, unaona, kuweka mambo yote pamoja. Kitu kingine ndiyo kwanza kiniguse moyo wangu, muda mchache uliopita. Nacho ni wakati shujaa mmoja mzee, mmoja wa mikono yake nusura ung'olewe na risasi, mguu nusura ung'olewe kwa risasi. Yeye hayuko hapa kunisikiliza sasa hivi. Lakini yeye ni mtu muungwana kweli, jina lake Roy Roberson, na mmoja wa wadhamini wetu hapa kanisani, na Mkristo mmoja muungwana. Alitokea pale tu, na kusema, "Ndugu Branham, usimsahau Rais." Kasema, "Ilinifanya nimsikitikie sana alipotokea," alimwona kwenye televisheni, "yeye akishuka kutoka kwenye ndege, huku machozi yakimtiririka mashavuni mwake, na kinywa chake kimeenda upande." Mwajua, alikuwako kule ng'ambo kabisa na Roy na hao wengine, katika vile—vile vita.

3 Si hoja kama unatofautiana naye katika siasa, yeye bado ni Rais wetu. Naam, bwana. Kwangu mimi, mimi—mimi si wa Democrat wala wa Republican. Mimi ni Mkristo. Lakini na—nawaambia, hakika nilimpenda sana Ra-Rais Dwight Eisenhower. Bwana, yeye hakika amekuwa mtu mmoja mkuu, jinsi ni-ninavyofikiria mimi. Kama alikuwa akigombea tena, nami nilikuwa ninapiga kura, ningempigia kura tena. Hiyo ni kweli. Sijali kama alikuwa—kama alikuwa na umri wa miaka mia moja, bado ningekuwa nikimpigia kura, kwa sababu ninampenda. Na hebu na tumkumbuke katika maombi yetu usiku wa leo. J. T., hakika ninaufurahia ule mkutano mzuri, ninyi nyote, ule uliokuwa nao wewe na Ndugu Willard juma hili. Kama ningaliingia kutokea nje, nyote mngelisema, "Vema, Ndugu Branham sasa, unajua, *fulani*." Lakini ni afadhali kusimama nje na kuwasikiliza, mnaona? [Ndugu Branham anacheka — Mh.] Vema.

4 Kwa hiyo, vizuri sana. Nina makanisa ninayotaka kuyatoa, kama nyote mnayataka, kama mko tayari kwenda kuanza kuwa wachungaji sasa, kama mmefunzwa. Na, jambo ambalo, naamini mmefundishwa, na mmetulia kabisa. Nina mmoja huko Oregon, mengine Washington, California, na Arizona, sehemu mbalimbali. Na kama ukitaka kuchukua kanisa ama cho chote kile, mbona, papa hapa ni mahali pazuri pa kuanzia, papa hapa. Na kuna watu wanaolia kila mahali, hata kule kwenye rizavu za Wahindi na popote unakotaka kwenda. Hebu utujulishe tu, kwa sababu ninaamini ninyi vijana mmekomaa sasa. Hiyo ni kweli. Napenda tu kuwaona wakifanya hivyo. Kuna Ndugu Ruddell kule juu barabarani. Nikienda kule kuhubiri katika mkutano wake, mnamo siku chache. Tutakuwa na uamsho, Ndugu Ruddell atakuwa nao. Nami na—nakumbuka nilikuwa nikimsukuma maskini jamaa huyo kila mahali, nikijaribu kumfanya ajivike lijamu na kuhubiri. Alikuwa mzito sana. Angesema, "Siwezi tu kuzungumza." Mnapaswa kumsikia. Amina. Unaona? Hujui unaloweza kufanya kama ukimwacha Roho Mtakatifu akushike. Hiyo ni kweli.

5 Na Ndugu Graham Snelling huko Utica, na Ndugu Junior Jackson kule chini. Tu—tunawahesabu wote kuwa makanisa yetu madogo, tunayoshirikiana nayo, yakiwa pamoja nasi. Sote tuko pamoja. Hatubishani juu ya mafundisho yetu, au matumaini yetu na malengo yetu, mafundisho yetu, ni kitu moja. Tunasimama pamoja, kila kitu pamoja. Sisi ni kanisa moja tu. Nasi hakika tungependa yasambae kila mahali; tuna mengine huko Afrika, mengine huko India, na kila mahali, kote nchini. Huko ndiko tunakoyataka yaweko, kutangaza Habari. Nami nawaona vijana hawa wakikua, kama Ndugu J. T. Parnell hapa, na—na Ndugu Willard na wengineo, wanapokua, vijana, ninapozeeka. Kama kuna kesho, watakuwa ndio hao watu wa kesho. Sitaki Ujumbe huu usife kamwe. Huiwezi kabisa. Haina budi kuendelea. Nami siamini tuna muda mrefu zaidi wa kuuleta. Yule mtoto mchanga waliyesema atakufa, naona umekuwa naye kanisani siku nzima leo, dada. Hilo ni jambo zuri sana. Tunamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo, kwamba Bwana ni mwenye neema, amejaa rehema. Endeleeni tu kuamini yale uliyoambiwa papa hapa, mnaona, itakuwa sawa.

6 Sasa, je! Mnafurahia mafundisho? Mnapenda mafundisho? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Loo, kweli na—na—nafikiri yanatusaidia. Yanatupa kupumzika kidogo kutokana na kuwaombea wagonjwa, na maono, na uponyaji wa Kiungu. Bila shaka, sasa, usiku wa leo sisi … Baada ya ibada, tutawaombea wagonjwa tena, usiku hii. Daima sisi hutaka kufanya hivyo, kumbatiza mtu ye yote wakati wo wote. Ni wangapi wanaokumbuka wakati nilipokuwa nikienda kuchunguza nyaya za umeme? Vema, nimetembea kupitia kwenye njia za umeme, mara nyingi, ilinibidi kutembea maili thelathini kwa siku porini. Ilinibidi kutembea umbali wa maili mia mbili themanini za kukagua njia za umeme. Ningesuka nipitie kule, shati

mikononi mwangu, na, loo, nimechoka sana, nikitemeba kwenye misitu hiyo, huku nachomwa na miiba ya mti mbichi. Nakutana na mzee fulani mkulima na kuketi chini ya mti na kuzungumza naye juu ya kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Angesema, "Vema, daima nimetaka kubatizwa." Nikasema, "Kijito hakiko mbali sana." Naye angesema … Nami nimechukua wengi wao moja kwa moja kule na kuwabatiza katika Jina la Yesu. Nikawapeleka moja kwa moja kufuatilia zile njia za umeme, upesi nilivyoweza kwenda. Hiyo ni kweli. Mara nyingi nikiwa nimevaa nguo zangu za kazi zilizochakaa, nikambatiza mmoja, nashuka moja kwa moja kutoka kwenye nguzo. Naketi kule juu nikifanya kazi juu ya nguzo; nilikuwa fundi wa nyaya za umeme, pia, nikifanya kazi juu ya nguzo, na mtu mwingine, huku nikimwambia habari za Bwana. Angesema, "Mbona, Billy, siku moja nitakuja kanisani mwako na nikabatizwe."

7 Ningesema, "Kwa nini unataka kungoja mpaka wakati huo? Tuko karibu sana na mto, kuna maji mengi mle." Washike sasa hivi. Hiyo ni kweli. Huo ndio wakati. Filipo alisema …

8 Yule towashi alimwambia Filipo, "Maji haya hapa, tunazuiwa na nini?" Hiyo ni kweli. Hakuna kitu. Kama uko tayari, huo ndio wakati. Usimwache Ibilisi apate nafasi ya kuingiza kitu fulani mle ndani. Usiahirishe mpaka kesho mambo ambayo ungeweza kufanya leo. Huenda kesho isije kwa ajili yako. Nakumbuka wakati mmoja nilifanya hivyo, nilijifunza, lilinipa somo. Niliahirisha jambo fulani ambalo nilipaswa kufanya siku moja, na kesho yake ilikuwa imechelewa sana.

9 Sasa, kweli sitaki kuwaweka wakati huu wote. Lakini mimi hu-huchomwa moyo sana, na, sijui, najisikia vizuri sana mpaka najisahahu, karibu najisahau. Ninajisikia tu vizuri sana.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo kabla hatujaliendea Neno.

Baba yetu wa Mbinguni, Wewe ni Mungu aliye hai, uishiye daima. Jua lililotua hivi punde, jua lile lile, Danieli aliliangalia lilipotua, Yeremia aliliangalia lilipokuwa likitua, Adamu aliliangalia likitua, Yesu aliliangalia likitua. Na ni ulimwengu ule ule walimoishi na kutembea ndani yake, na Wewe ungali u Mungu yule yule.

Usiku huu kuna haja nyingi. Mtu mmoja mwenye uvimbe kwenye ubongo, dada fulani anahofia jambo lile lile. Wewe ndiwe tumaini pekee, Bwana, lililopo kwa ajili ya jambo hilo. Uvimbe huo umekuwa wa kufisha, hakuna kinachoweza kuukomesha. Hauko kwenye uwezo wa daktari kabisa. Lakini usiku wa leo tunaenda na kombeo letu dogo, tukimwendea huyo mwana-kondoo, kumrejesha kwenye zizi la Baba. Katika Jina la Bwana Yesu tunaelekeza maombi yetu kusudi tumwue huyo simba, huo uvimbe, uletao mauti, kuwaleta salama kwenye zizi.

10 Nasi, Mungu, tunamkumbuka usiku wa leo Rais wetu mpendwa, ndugu, Dwight Eisenhower wetu. Ameiongoza nchi, Bwana, amejaribu kutuepusha na vita. Aliahidi vile vita vya Korea vingeisha kama angekuwa kwa njia yo yote. Yeye aliwaahidi hao akina mama angewarudisha hao vijana wavulana. Lakini yeye alisema, "Kwangu mimi kufanya jambo hilo, siwezi. Naweza kuweka juhudi zangu, lakini Mungu pekee ndiye atakayetenda hilo." Nawe ulikuwa pamoja naye, Bwana, na sasa yote yamekwisha. Mbona hawakuweza kuona jambo hilo hapo awali? Mungu, naomba kwamba utamsaidia. Mbariki mtu huyo shujaa, Bwana. Nasi tunaomba kwamba utatuchagulia kiongozi atakayemfuata. Mapenzi Yako ya kuchagua tangu zamani yatendeke, Bwana.

Lakini Yule ambaye anatuvutia sana naye usiku wa leo, mbali na mambo yetu ya kitaifa, ni Yule aliye mkuu na mwenye utukufu anayekuja kuanzisha Ufalme ambao hautakuwa na mwisho, Bwana Yesu, Mwanao. Ndipo watazirundika zana za vita, ngoma zitalia na hakutakuwa na vita tena. Watapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake. Watajenga nyumba, waishi ndani yake. Na hakutakuwa na shida tena basi baada ya hayo.

Tubariki sasa tunapoliendea Neno. Na, Baba, Wewe unajua sababu ya mimi kuliendea Neno kutoka kwenye Andiko hili hili hapa. Ni kwa sababu kwamba na—najisikia ya kwamba Wewe unanitaka nilitende jinsi hii, kwamba ni mapenzi Yako ya Kiungu, liko katika utaratibu Wako, liko katika … liko katika utaratibu wa siku, kuwaacha watu waone mahali pao nao waweze kuwa tayari kwa ajili ya saa ya vita. Kama vile ndugu yetu alivyosema katika maombi yake Kwako si muda mrefu uliopita, "Loo, Wewe umetufunza kwa muda mrefu sana, Bwana." Sasa, Baba, tupe vyeo vyetu. Tuweke huko nje kwa yale tunayopaswa kufanya, kusudi tuweze kuwa katika kazi ya Baba. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

11 Kwa namna fulani nilikuwa na alasiri nzuri sana hii alasiri ya leo, nikizungumza na daktari maarufu huko Louisville, nesi wake. Walisikia habari za mambo matukufu ya Bwana. Na baba yake alikuwa daktari. Naye akaja na kuketi chumbani mwangu karibu alasiri yote, akaingia tu, akaingia ndani. Mtu mzuri sana; mgumu kidogo, mwajua, kwa namna fulani ni Mpresbiteri thabiti, mwanzoni, lakini aliondoka huku machozi yakitiririka mashavuni mwake. Loo, mimi … Mungu anao wakitokeza tu kila mahali, katika ofisi za madaktari, kwa manesi. Siamini kuna nesi katika Hospitali ya Wagonjwa ya Norton ambaye sikumshuhudia juu ya kumpokea Roho Mtakatifu, na kumwuliza kama alikuwa amebatizwa katika Jina la Yesu. Hakuna daktari niliyekutana naye, mahali popote, ama haku- … Unaona?

Waambieni habari Zake. Hatuna wakati mwingi, ndugu. Haidhuru inaonekana ni ngumu jinsi gani hapa, ngojeni tu mpaka mtakapovuka pumzi hiyo ya mwisho kule na muone, ndipo mtatamani mngefanya hivyo. Naam, bwana. Usingoje mpaka wakati huo, hebu na tufanye hivyo sasa hivi. Wakati ndio huu. Loo, huenda wasikubaliane, na kukasirikia na kuzozana kidogo juu ya jambo hilo, bali hawamaanishi jambo hilo. Kwa kweli hawamaanishi jambo hilo. Wao—wao—wao wako sawa. Wanapoanza kubishana na wewe, kumbuka tu—kumbuka tu, wao—wao hawamaanishi jambo hilo. Hawamaanishi hilo. Labda lwao wamefundishwa jambo fulani nao wanalishikilia tu hilo, kwa hiyo u—unaweza kuona wazo lao. Usibishane nao, usibishane na mtu ye yote, bali wapende tu hata walipokee Hilo. Kisha uwaombee.

12 Vema, nafikiri tulifikia kwenye aya ya 9, sina hakika. Hiyo ni mbali sana na ile sura ya 3, sivyo, enyi watu? Lakini loo, ni asali mwambani, kwangu mimi! Tulikuwa tukizungumza sasa, kumbukeni, ili tuweze kupata msingi mdogo tena. Na sasa, Ndugu Neville, u—univuta kidogo sasa kama nikishindwa kuona wakati ukiisha, ili niweze kuwaombea wagonjwa. Tunataka kupata kila chembe ndogo tuwezayo. Na usiku wa leo nataka wito wa madhabahuni. Mimi … Kumaliza kwa jambo hili ambalo naweza tu nikasoma yaliyosalia.

Lakini kusudi la jambo hili, ni, kuona mahali pako katika Kristo, kuona kwamba si kitu tu ulichoangukia, ama kitu fulani ambacho huenda kilikuwa … ulikistahili mahali fulani, bali ni kile Mungu alichokutendea, Yeye Mwenyewe. Si kwamba ulikuwa mzuri sana hata ukaenda kanisani usiku mmoja, hivi kwamba maskini ndugu fulani alikuongoza madhabahuni. Na haikuwa hivyo. Ilikuwa ni Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuchagua tangu zamani uapte Uzima wa Milele. Unapofika kule siku ile, si ajabu wale arobaini … wazee ishirini na wanne walivua taji zao, kila mtu alivua taji yake, kila mtu akaanguka kifudifudi, hawakuwa na jambo moja waliloweza kusema, hakuna mhubiri, hakuna mzee, hakuna chochote. Sifa zote kwa Mwana-Kondoo! Mungu atakusanya katika Yeye vitu vyote siku hiyo. Loo, laiti tungelimjua na kumtambua Huyo waliyemsulubisha alikuwa Nani. Sasa kwenye …

13 Tunaanzia kwenye aya ya 8, kili upata msingi mdogo.

> *Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi;*
>
> *Akisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, …*

“Siri za mapenzi Yake.” Basi mnakumbuka jinsi tulivyoshikilia hayo? Ni wangapi waliokuwa hapa asubuhi ya leo, hebu tuone. Jinsi tulivyoshikilia hayo, “siri ya mapenzi Yake.” Sasa, si ati jambo dogo tu, halafu ni siri. Mapenzi ya Mungu ni siri. Na kila mtu hana budi kutafuta mapenzi ya Mungu kwa ajili yake mwneyewe, mwanamume kwa mwanamke, fumbo la Mungu.

Tunapataje? Paulo, aliyajua. Yeye alisema hakufanya shauri na mtu ye yote, hakuna cha mtu wa nyama na damu. Yeye hakwenda shule yoyote, wala seminari. Hakuwa na uhusiano wowote nayo. Lakini yeye … Ilifunuliwa kwake na Yesu Kristo, Ambaye alikutana naye njiani akienda Dameski, katika—katika Nuru kama Nguzo ya Moto, Nayo ikamwita. Naye akaenda Arabuni, na huko akakaa miaka mitatu. Loo, hivi hudhani huo ulikuwa muda mrefu, Ndugu Egan? Miaka mitatu Paulo kule Arabuni, alipangisha jengo dogo mahali fulani, akitembea huku na huko sakafuni, akiwa na magombo yote ya kale. Hawakuwa na yale mapya; Paulo ndiye aliyeyaandika, karibu yote. Humu ndani ya magombo haya ya kale, jinsi ambavyo Mungu, hapo mwanzo, alituchagua tangu awali kwa ajili ya Uzima wa Milele. Jinsi ambavyo angemtuma Yesu, ili kwamba kupitia Dhabihu hii sote tupate haki ya ule Mti wa Uzima. Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; hao aliowaita, tayari amewahesabia haki; hao aliowahesabia haki, tayari amewatukuza. Mungu, tangu mwanzo wa ulimwengu, alitangulia kutuchagua tupate kufanywa wana wenye mamlaka. Sasa viumbe vyote vinaugua, vikingojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu. Loo, ningemwazia Paulo alikuwa na wakati mzuri sana. Ningependa kuwa kule pamoja naye. Na wewe je?

14 Sasa yeye alisema, “Alitujulisha lile fumbo.” Upate Roho Mtakatifu wakati fulani, na uanze kuendeleza Hilo na uangalie tu jinsi inavyoenda. Alasiri ya leo nilikuwa na, loo, kama dakika thelathini za kusoma, kupitia tu somo hili; labda sivyo, ningesema nusu ya hizo, kama kwenye dakika kumi na tano katikati ya nyakati. Nami nikaanza kulifuatilia, nikawaza, “Lile fumbo, ni ya kimafumbo iliyoje!” Na Maandiko yalinirudisha katika Agano la Kale, kisha yakanirudisha kwenye Agano Jipya; yakafumanganisha mambo fulani pamoja, kuona lile fumbo la Kuja Kwake, fumbo la mapenzi Yake, lile fumbo la sisi kuketi pamoja. Kumbuka, haiwezi kufundishwa katika seminari yoyote. Ni fumbo. Huwezi kulijua kwa njia ya elimu, kwa njia ya theolojia. Ni fumbo lililofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, likingojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu.

15 Niambie, ndugu yangu, niambie, dada yangu, ni wakati gani ambapo wana wa Mungu walipaswa kudhihirishwa nje ya wakati huu sasa? Ni lini kuliwahi kuwako na wakati katika historia, walipodhihirishwa katika wakati wa kuyakomboa viumbe vyote? Viumbe, viumbe vyenyewe vinaugua, vikingojea ule wakati wa kudhihirishwa. Mbona, kabla ya ule upatanisho kufanywa, kabla ya Roho Mtakatifu kumwagwa, kabla ya Agano la Kale lo—lote, na kuendelea huko kote, hakungaliweza kuwa na kudhihirishwa. Kulipaswa kungoje mpaka wakati huu. Sasa mambo yote yamekwishaletwa, yakija, yakielekea kwenye jiwe la kichwani, kufikia kule kudhihihirishwa kwa wana wa Mungu, na Roho wa Mungu akiingia ndani ya hawa

watu, kikamilifu sana, hata huduma yao itafanana sana na ya Kristo hata itamuunganisha Yeye na Kanisa Lake pamoja.

16 Ni wangapi waliopata kusoma historia ya piramidi? Nadhani labda bibi mmoja hapa aliinua mkono wake. Vema.

Mungu aliandika Biblia tatu. Moja ya hizo ilikuwa ni Zodiaka angani, hiyo ndiyo Biblia ya kwanza. Mwanadamu alipaswa kuangalia juu ili kutambua kwamba Mungu anatoka juu. Fuatilia Zodiaka, je, uliwahi kuichunguza? Hata inaonyesha kila wakati, hata wakati wa kansa. Inaonyesha hapo mwanzo, kule kwa-… kuzaliwa kwa Kristo. Umbo la kwanza katika Zodiaka ni nini? Bikira. Umbo la mwisho ni nini? Leo yule simba. Kule Kuja kwa kwanza na Kuja kwa pili kwa Kristo, yote yameandikwa humo.

Ndipo Biblia iliyofuata iliyoandikwa, ilikuwa ni kwneye mawe, yanayoitwa "mapiramidi." Mungu aliandika katika yale piramidi. Kama ukiyachunguza, angalia zile historia za kale pamoja na vita, jinsi yalivyojengwa kabla ya yale maangamizi ya siku za gharika.

17 Ya tatu iliandikwa kwenye karatasi, Biblia, kwa ajili ya ulimwengu mkuu ujao, wa wenye akili na walioelimika. Sasa, kwa kuwa Mungu amepiga hatua katika nyakati zote, tuko kwenye Leo yule simba. Tuko kwenye kule kuwekwa jiwe la kilele cha piramidi. Tuko katika Kitabu cha Ufunuo, penye ile sura ya mwisho. Sayansi inasema tuko dakika tatu kabla ya usiku wa manane. Loo, wazieni mahali tulipo.

Na angalieni, hebu tuchukue piramidi, ni rahisi. Iko katika umbo kama la pembe tatu.

Wakati tulipokuwa hapa chini mwanzoni kwenye wakati wa mwanzoni wa kanisa, baada ya yale Matengenezo katika wakati wa Luther, kwa mtu kusema tu yeye alikuwa ni Mkristo, aidha angeokoa maisha yake ama auawe. Walimwua kwa hata yeye kusema alikuwa Mkristo. Kwa hiyo kupitia mateso … Kila kipindi, katika kila wakati, kumekuwa na mateso. "Wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu watateswa." Katika wakati wa Luther, lilikuwa ni jambo la kutisha kusema "Mlutheri." Ulichukuliwa kuwa mshupavu wa dini, na ungeweza kuuawa. Mara nyingi waliwaua kwa kuwafungia kwenye nguzo, wakawateketeza kwa moto, na kila kitu kingine, kwa kuwa Walutheri.

18 Ndipo kanisa likapungua upana, kama vile piramidi. Llifikia hatua nyingine ya neema, ambayo ilikuwa utakaso. Wakati wa Wesley, wakati alipolipinga kanisa la Kianglikana, akafundisha utakaso. Likafikia katika uchache wa watu tena, ndipo wakaitwa kundi la washupavu wa dini.

Ni wangapi humu ndani waliokuwa Methodisti, ama waliowahi kuwa, ama waliwahi kuunganishwa na kanisa la Kimethodisti? Nusu yenu. Je! Mlijua kwamba kanisa la Methodisti karibu limpate Roho Mtakatifu wakati mmoja? Nimehudhuria kwenye makanisa ya Kimethodisti na kuwaona wakianguka sakafuni, nao wakawamwagia maji katika nyuso zao na kuwapepea kwa feni, kumzuia Roho Mtakatifu asiwashukie. Hiyo ni kweli. Sasa, hiyo ni kweli, kule chini kwenye vilima vya Kentucky ambako tulikuwa na Wamethodisti. Ninyi watu ni wajiungao na kanisa huku nje. Tulikuwa na Wamethodisti kule nyuma, na Wabaptisti. Tulipiga magoti madhabahuni na kupigana-pigana mgongoni sisi kwa sisi mpaka tukapata kitu fulani. Tulipomaliza, tukaishi tofauti baada ya hayo.

Lakini wewe unakuja tu na kuandikisha jina lako kwenye kitabu na kusema, "Mimi ni Mmethodisti." Na wanachukua kopo la chumvi na kukunyunyizia maji kidogo, na ndiyo basi. Mnaondoka mnaenda na kuvaa kaptura, kujipodoa, mnaingia kwenye mashindano ya farasi, manwekeana bahati nasibu, mnacheza kamari, mnacheza mchezo wa kubahatisha na kila kitu kingine, mngali Wamethodisti wazuri, mnaona. Hiyo si Methodisti. Hao ni wajiungao na kanisa tu. Hiyo ni kweli. Mbatisti, vivyo hivyo, Mpresbiteri, na kuendelea vivyo hivyo.

19 Kama vile David duPlessis alivyosema, "Wajukuu, Mungu hana wajukuu wo wote." Mungu kamwe hajawahi kuwa na mjukuu. Yeye anao wana, bali si wajukuu wa kiume. Hiyo ni kweli. Ninyi … na watu waliokuja katika kanisa la Kimethodisti, ama kanisa la Kipentekoste, ama kanisa la Kibaptisti, kwa sababu mama yako au baba yako alikuwa Mpentekoste au Mbatisti, basi wewe ni mjukuu. Hao walikuwa wana. Wewe ni mjukuu, unaona. Kwa hiyo Mungu hana kitu kama hicho. Kanisa lina wengi sana wa hao, lakini si —bali si—si—si … Mungu hana.

20 Sasa, angalieni haya, inashuka moja kwa moja mpaka inafikia chini sasa, inafikia uchache, wa kanisa. Wakati wa Kipentekoste ukaingia. Huo bila shaka ulikata vivimbe vingi sana. Ndipo ukafanyanje? Ukamwacha tu Mmethodisti na Mluteri nyuma kabisa.

Sasa Roho Mtakatifu alipiga hatua akauacha wakati wa Kipentekoste. Walifanya nini? Waliunda dhehebu, wakajifanya wenyewe, "Sisi ni Assemblies of God. Sisi ni wa Umoja. Sisi ni wa Uwili. Sisi ni wa kanisa la Mungu. Sisi ni "hili*, ama* kile*. Wewe si mfuasi, huwezi kuingia Mbinguni isipokuwa jina lako liwe limeandikwa kwenye kitabu chetu." Loo, upuuzi kama huo! Sijali kama wewe ni Mbatisti, Mmethodisti, Mpresbiteri, unaandika jina lako kwenye Kitabu cha Uzima wakati Mungu anapoliweka pale. Kama ulikuwa umechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya Uzima wa Milele, Mungu atakuita kwa njia fulani, kwa namna fulani, kwa—kwa njia fulani ama nyingine. Hakika atakuita. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu."

Haidhuru wewe ni wa kanisa gani, hilo halina uhusiano wowote nalo. Lakini dhehebu kamwe halitakusaidia kwa lolote, bali huenda likakuzuia sana kuambatana na Mungu, bali ha—halitafanya jambo lingine kamwe. Linakusanya pamoja na kundi la waaminio na wasioamini. Bila shaka, unakutana na hilo kila mahali uendako, na hata walikuwa na jambo hilo Mbinguni. Kwa hiyo, ni sawa, bali unategemea dhehebu lako. Mtegemee Yesu, Yeye Ndiye wa kutegemewa.

21 Sasa tunapokuja moja kwa moja kufikia … wao walikuwa … Ni wangapi … Ninaamini mwanamke huyu hapa aliinua mkono wake juu, kwamba alikuwa umejifunza juu ya mapiramidi. Mwajua, piramidi halijafunikwa kamwe. Sivyo? Kamwe halikuwekewa lile jiwe la kileleni. Hawakufanya hivyo kamwe, hata hawakuweza kulipata hilo. Hawajui hata kilicholipata. Kwa nini? Kwa nini lile jiwe la kileleni halikuwekwa juu yake, lile jiwe la kileleni, jiwe la kifuniko? Kwa sababu Yeye alikataliwa wakati alipokuja. Yeye alikuwa lile Jiwe lililokataliwa. Hiyo ni kweli. Lakini litawekwa kifuniko. Hiyo ni kweli. Na kisha hayo mawe yanayoenea kulizunguka hilo Jiwe la Kuweka Juu, hayana budi kuwa ni mawe ambayo yatafanana kabisa na Jiwe hilo, yatakayoenea, kuungana na kila—kila mahali. Hiyo piramidi ni kamilifu sana hata huwezi kuingiza wembe kati yake, mahali mawe hayo yanakoshikana pamoja. Ni uashi mzuri jinsi gani. Baadhi ya hayo yangekuwa na uzito wa mamia ya tani kadha huko juu hewani, nayo yameshikamanishwa pamoja kikamilifu sana.

22 Hivyo ndivyo Mungu anavyolileta Kanisa Lake. Tumeunganishwa sawasawa pamoja, moyo mmoja na nia moja. Sasa mtu fulani anasema, "Vema, Walutheri huko nyuma hawakuwa na kitu." Msiliamini jambo hilo. Walutheri watafufuka katika ule ufufuo kama tu vile hao wengine watakavyofufuka katika ule ufufuo. Wabatisti, Wapresbiteri, na watoto wote wa Mungu, watafufuka katika ule ufufuo. Na hiyo ndiyo sababu leo watu husema, "Loo, vema, patatokea uamsho motomoto ambao utatokea hapa na uende kuwaokoa Wapentekoste milioni mia moja. Wote wataokolewa na kisha kutakuwako na Kunyakuliwa." Umekosea. Huko kunyakuliwa kutakuwa ni mamia ya maelfu, hiyo ni kweli, lakini hao wanatolewa katika miaka elfu sita ya wokovu pia, miaka elfu sita huko nyuma. Mtu hutembea katika Nuru jinsi Nuru inavyomjia, yeye anavuka madaraja wakati anapoyafikia. Sasa, kama akiikataa, basi anaachwa gizani. Lakini kama akiendelea kusonga mbele!

23 Sasa, tazama, basi kule Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia sana hata Roho kutoka kwenye kina cha ndani kabisa humu … kufikia tu kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na sasa kufikia wakati wa kuja kwa lile Jiwe la Kuweka Juu. Kanisa halina budi kufanana kikamilifu kabisa na Kristo hadi Kristo na Kanisa waweze kuungana pamoja, Roho yule yule. Na kama Roho wa Kristo yumo ndani yako, anakufanya uishi maisha ya Kristo, kutenda maisha ya Kristo, kufanya kazi za Kristo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Yesu alisema hayo. Unaona? Sasa tutakuwa na, tuna huduma inayokuja ambayo inafanana kabisa na maisha ya Kristo. Huduma hiyo inatambulisha nini? Kuja kwa Bwana.

Liangalie hilo ulimwenguni leo, na uone yale Khrushchev anayosema, mambo haya mengine yote makuu, na mizozo mikubwa ulimwenguni kote ilnavyokaribia, wakati wo wote, ingeweza kuwa unga sekunde yoyote. Hiyo ni kweli. Na kama ndivyo, tunajua ya kwamba hilo linakaribia. Mtu ye yote mwenye akili anaweza kusoma katika gazeti ama kusikiliza redio, na kujua kwamba jambo hilo limekaribia. Vema, kumbukeni, Kristo anakuja kwa ajili ya Kanisa Lake kabla jambo hilo halijatukia. Kwa hiyo Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia namna gani? Labda kabla mkutano huu haujaisha usiku huu. Tuko katika wakati wa mwisho. Ni kweli hakika.

24 Angalia jinsi kanisa limekuja, linavyosonga mbele. Hebu liwazieni katika nia zenu, ninyi wanahistoria mnaosoma historia. Angalia kanisa la Kiluteri chini ya kuhesabiwa haki, likitoka tu katika Ukatoliki likiwa jipya, liangalieni likisonga mbele. Kisha mwangalieni Wesley akikaribia kidogo, katika utakaso, akipitia katika Maandiko. Angaliani papo hapo katikati, yule Wesley. Ndipo kitu kilichofuata kilikuwa ni wakati wa Kipentekoste. Na wakati wa Pentekoste ukiwa ni kurejeshwa kwa karama, karama za kiroho. Sasa, angalieni ule wakati unaokuja sasa hadi kwenye lile Jiwe la Kuweka Juu. Mnaona ninalomaanisha? Kuja kwa Bwana, kufunuliwa. Mungu pamoja na viumbe vyote anangojea kanisa lipate mahali pake.

25 Shida yak leo, mimi … karibu kila mtu niliyekutana naye. Nilikuwa nimevingirishwa, tulikuwa tukifanyiwa … Sina budi kupimwa afya, mwajua, kama tunasafiri kwenda nchi za ng'ambo, ninyi wamishenari na kadhalika mnajua jambo hilo. Nilipokuwa nikipimwa afaya walinitoa kwenye kile chumbani pale, nilikuwa nikinywa maskini … ilionekana kwangu kama namna fulani ya uji, ama unga, ama kitu fulani, nami—nilikuwa nikinywa. Nami nikaja pale, nikaketi chini, nikangojea kwa nusu saa nione kama itatoka tumboni mwangu au la. Nikaangalia upande wa pili, na kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, ilionekana kana kwamba alikuwa anakaribia tu kufa. Alikuwa ninii sana … miguu minyonge na mikono minyonge. Nami nikaendelea kwenda kutoka kwa mwanamume huyu kwenda kwa mwanamume yule, kutoka kwa mwanamume huyu kwenda kwa mwanamume yule, nikizidi kumsogelea yule mwanamke, mpaka nikamfikia mahali alipokuwa. Alionekana kama maskini kitu dhaifu kinachokaribia kufa. Nami nikamkaribia, nikasema, "Samahani, mama."

Akasema, "U hali gani?" Loo, alikuwa mgonjwa sana!

Nami nikasema, "Kuna shida gani?"

Akasema, "Nilienda Tucson kumtembelea binti yangu. Nikaugua, hawawezi kujua ni shida gani."

Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo moja." Nikasema, "Mimi ni mhubiri wa Injili. Je! Wewe ni Mkristo? Uko tayari kwenda kama saa hiyo itafika?"

Naye akasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa *fulani*."

Nikasema, "Hilo halikuwa swali nililokuuliza. Je! Wewe ni Mkristo aliyejazwa na Roho wa Mungu na uko tayari kwenda atakapokuita?" Yule mwanamke hata hakujua nilichokuwa nikizungumzia. Unaona? Loo, ni hali ya kuhuzunisha jinsi gani ulimwengu ulivyo!

26 Sasa, "kujulisha mafumbo ya mapenzi Yake," kule kuja … Hebu niwasomeeni jambo fulani. Nilikuwa nikisoma kwenye … Hebu tufungue sasa kwenye "fumbo la mapenzi Yake." Hebu tufungue Waebrania hapa kwa muda kidogo tu, ile sura ya 7 ya Waebrania, naamini ndipo penyewe. Nami ningetaka kuwasomea jambo fulani ambalo lingewafanya tu mjisikie vizuri sana tunapowazia juu ya sisi kuketi pamoja katika maeneo ya Kimbinguni. Waebrania, sura ya 7.

> *Kwa maana Melkizedeki huyo,* (sasa angalia) *mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, …*

27 Fumbo ni nini sasa? Fumbo ndilo hili, angalia hili. Jamaa huyu ni nani, "afanyaye, akijua, fumbo la mapenzi Yake," huyu Melkizedeki? Ninamngojea kila mtu hapa, Biblia zingali zinafunguliwa. Waebrania, sura ya 7, Paulo akinena, mtu yule yule kwa Wagalatia.

> *Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu Aliye juu, … aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;*
>
> *Ambaye pia Ibrahimu alimgawia sehemu, sehemu* fulani, *sehemu ya kumi ya vitu vyote; tafsiri* ya jina lake kwanza ni *Mfalme wa haki,* tena ... Mfalme wa Salemu, *(Jamaa Huyu ni nani?)* maana yake, Mfalme wa amani;*
>
> *Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake; …*

28 Mtu huyu alikuwa ni nani? Yeye alikuwa ni nani? Yeye kamwe hakuwa na baba, kamwe hakuwa na mama, kamwe hakuwa na wakati alipoanza, wala hakuwa na wakati atakaokufa. Alikutana na Ibrahimu akija kutoka kuwapiga hao wafalme. Alikuwa akifanya nini? Alitoka kwenda kumleta Lutu, ndugu yake aliyepotea, kumrudisha. Naye akawapiga hao wafalme; ambao, hao wafalme ambao alikuwa amewapiga; naamini wafalme kumi ama kumi na watano, na falme zao. Lakini Ibrahimu aliwapa silaha watumishi wake akaenda kumfuatilia, akajitenga peke yake usiku, unaona, wakati alipomshika wakati wa usiku. Loo, ndugu, tunafanya kazi gizani sasa, Nuru pekee tuliyo nayo ni Nuru ya Injili. Lakini alijitenga peke yake, kisha akampata na kumrudisha. Na alipokuwa akirudi, baada ya vita kwisha!

Hebu twendeni kwenye Mwanzo 14, kwa muda kidogo tu, tuipate hiyo habari kwa dhahiri zaidi. Hebu twendeni hapa katika Mwanzo, ile ya nne- … Naamini ni ya 14, Mwanzo 14. Naam, hebu na tuchukue Mwanzo 14:18, tuanze. Hebu tuanzie nyuma kidogo ya hapo. Hebu tuanzie, naam, aya ya 18, Mwanzo 14:18, "Naye Melkizedeki …" Sasa, huyo ni Ibrahimu akirudi sasa kutoka kuwapiga hao wafalme. Akarudi, alipokuwa akirudi, akimrudisha Lutu, watu wote waliokuwa wamewateka. Wote!

29 Kama vile Daudi, ambaye aliondoka akaenda na kuleta … Daudi alifanya nini? Alichukua lile kombeo dogo, akatoka akaenda akamnyakua maskini mwana-kondoo huyu kutoka katika kinywa cha simba. Wazia juu ya kombeo, akimtafuta mwana-kondoo. Ni nani ulimwenguni angefanya hivyo? Niambieni ni mtu gani humu ndani atakayefanya hivyo, inua mkono wako juu. Nitakwambia upesi sana kwamba umekosea. Hukuniona mimi nikiinua wangu juu. La, nisingemwendea nikiwa na bunduki ya thelathini-sifuri-sita, ni vigumu. Lakini yeye alimwendea kwa kombeo, kipande kidogo cha kitu kama ngozia, chenye kamba mbili, kukizungusha-zungusha. Kwa sababu … Na ilipofika wakati wa Goliathi kujigamba, akamwendea Goliathi, naye akasema, "Mungu wa Mbinguni ameniwezesha kumwokoa mwana-kondoo kutoka kwenye kinywa cha simba, kutoka kwenye kinywa cha dubu." Alijua haikuwa kombeo. Ilikuwa ni nguvu za Mungu zilizoandamana naye. Ndiye aliyemrudisha huyo mwana-kondoo.

30 Na hivyo ndivyo tunavyosema leo. Mungu anao akina Daudi walioko kila mahali, naam bwana, wanaowalisha kondoo wa Baba. Na mara kwa mara uvimbe utakuja, ama kansa itakuja, ama cho chote kile, na kimshinde daktari kabisa. Hilo halitamzuia huyu Daudi, yeye atatoka aende moja kwa moja akamfuatilie jamaa huyo, na kombeo dogo, la, "Ombeni lo lote katika Jina Langu, nanyi mtapewa." Sijali, madaktari wanaweza kucheka, na kila mtu mwingine anaweza kumdhihaki, atamfuatilia hata hivyo, akimrudisha huyo kondoo kwenye zizi. Naam, bwana. "Yeye ni mtoto wa Mungu, ondoa mkono wako kwake!" Akamwangusha huyu simba chini, kisha huyo simba akainuka, akamshika ndevu na kumwua;

maskini kijana mdogo mwekundu, labda alikuwa na uzito wa ratili themanini au tisini.

31 Angalia. Melkizedeki, Mfalme wa Salemu ambaye ni Mfalme wa Amani, ambao Salemu hasa uko upande wa pili wa kilima. Ni Mfalme wa Yerusalemu, ndivyo alivyokuwa. Huyo ndivyo alivyokuwa hasa, Mfalme wa Yerusalemu. Ambao, Yerusalemu kwanza uliitwa Salemu, ambalo ni amani; huo ulikuwa Yerusalemu kwanza, kabla haujaitwa Yerusalemu. Yeye alikuwa Mfalme wa Yerusalemu. Yeye alikuwa Mfalme wa haki, Mfalme wa amani, Mfalme wa Salemu. Hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku zake, hakuwa na mwisho wa maisha, hakuwa na ukoo. Loo, loo, loo! Jamaa huyu ni nani? Mwangalie. Baada ya vita kwisha, baada ya ushindi kupatikana, angalia alichosema. "Naye Melkizedeki," aya ya 18, sura ya 14, Mwanzo.

> *Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai; naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana.*
>
> *Akambariki, akasema, Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba wa mbingu na nchi.*
>
> *Na ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mkononi mwako. Abrahamu akampa fungu la kumi la vitu vyote.*

Hebu na tusome zaidi kidogo.

> *Mfalme wa Sodoma akamwambia* Ibrahimu, *Nipe mimi hao watu, na hizo mali uchukue wewe.*
>
> *Abramu akamwambia mfalme wa Sodoma, Nimeinua mkono wangu kwa BWANA, Mungu aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi,* (Sikilizeni jinsi alivyofupisha hayo, hum, jinsi alivyomwambia!)
>
> *Ya kuwa sitatwaa nyuzi wala gidamu ya kiatu, wala sitachukua kitu cho chote, wala cho chote kilicho …* na waweza kusema, na *kilicho chako, usije ukasema, Nimemtajirisha Abramu;*
>
> *Isipokuwa hivyo vijana walivyokula, …*

32 Mwangalie huyu Melkizedeki mara tu alipokutana na Ibrahimu akitoka kuwapiga hao wafalme. Fumbo la Mungu sasa likifunuliwa! Yeye alikuwa ni nani? Hakuna mtu … Hawawezi kupata historia yo yote Yake, kwa sababu hakuwa na baba ye yote, hakuwa na mama ye yote, kamwe hakuwa na mwanzo wo wote wa wakati wake, kamwe hakuwa na wakati wo wote angekufa, kwa hiyo hata awe Nani Yeye bado angali hai. Yeye kamwe hakuwa na mwanzo, hivyo asingeweza kuwa mwingine ila El, Elah, Elohimu; aishiye peke Yake, adumuye peke Yake, Mwneyenzi Mungu!

Yesu alikuwa na Baba, Yesu alikuwa na mama; Yesu alikuwa na mwanzo wa siku, Yesu alikuwa na mwisho wa uhai wa duniani. Lakini Mtu huyu hakuwa na baba wala mama, amina, hana baba wala mama. Yesu alikuwa na Baba na mama pia. Mtu huyu hakuwa na baba wala mama. Amina. Naye alifanya nini, baada ya vita kwisha, baada ya Ibrahimu kuchukua mahali pake?

Baada ya kanisa kuchukua mahali pake, tunaitwa tupate kufanywa wana wenye mamlaka, kwa njia ya Roho Mtakatifu. Na wakati kila mtu anapochukua mahali pake, kile Mungu amemwitia kufanya, na kusimama kwenye mwisho wa safari, akiwafuatilia waliopotea.

33 Kwanza, Paulo anaondoa woga wote kutoka kwenye hilo, kwa hiyo sasa, "Kama umeitwa, iwapo wewe husukumwi na namna fulani ya theolojia, kama kweli umezaliwa na Roho, basi Mungu alikuchagua tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, akaliandika jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, na sasa tunakusanyika pamoja kuketi katika maeneo ya Kimbinguni katika Kristo Yesu. Watu watakatifu, taifa takatifu, watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, tukitoa dhabihu za kiroho kwa Mungu, yaani, matunda ya midomo yetu ikilisifu Jina Lake."

Watu huingia na kusema, "Hao watu wana kichaa." Hakika ni vichaa; hekima ya Mungu ni upumbavu kwa mwanadamu, na hekima ya mwanadamu ni upumbavu kwa Mungu. Zinahitilafiana, moja kwa nyingine.

34 Lakini kanisa halisi lililojazwa na Roho, lililojaa nguvu za Mungu, likiketi pamoja katika meneo ya Kimbinguni, likitoa dhabihu za kiroho, sifa za Mungu, Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwao, akizitambua dhambi na kutangaza mambo yaliyo mabaya miongoni mwao, akiyanyoosha na kuyalainisha yawe usawa. Kwa sababu nini? Daima Uweponi mwa Mungu kuna ile Dhabihu iliyotapakaa damu.

Sasa kumbukeni, tuliyapitia hayo asubuhi ya leo. Hukuokolewa kwa Damu, unahifadhiwa uliyeokolewa kwa njia ya Damu. Bali uliokolewa kwa njia ya neema, kupitia imani, ukiiamini Hiyo. Mungu alibisha hodi moyoni mwako kwa sababu alikuchagua tangu zamani. Uliinua macho yako juu na ukaiamini, ukaikubali.

Sasa Damu inafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zako. Kumbukeni, nilisema, "Mungu hamhukumu mwenye dhambi kwa ajili ya kufanya dhambi." Yeye kwanza ni mwenye dhambi. Yeye humhukumu Mkristo kwa kutenda dhambi. Halafu basi kwa sababu amemhukumu, Kristo alichukua hukumu yetu. Kwa hiyo hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kwa kuufuata mwili, bali kwa jinsi ya Roho. Na kama ukifanya jambo lo lote baya, si kwa makusudi. Hutendi dhambi makusudi. Mtu anayetenda dhambi makusudi, anatoka na kutenda dhambi makusudi, bado hajaingia katika huo Mwili. Lakini mara mtu anapoingia mle, amekufa, na uhai wake umefichwa katika Mungu, kwa njia ya Kristo, akatiwa muhuri nakw anjia ya Roho Mtakatifu, na Ibilisi hata hawezi kumpata, yuko kule nyuma kabisa. Itambidi atoke mle kabla Ibilisi hajampata. "Kwa maana umekufa!"

35 Mwambie mtu aliyekufa kwamba yeye ni mnafiki na uone kitakachotukia. Mpige teke ubavuni na useme, "wewe maskini mnafiki, wewe," hatasema neno. Na hiyo ni kweli, atakaa tu pale.

Na mtu aliyekufa katika Kristo, unaweza kumwita mnafiki, umwite cho chote unachotaka kumwita, yeye kamwe hatainuka juu ya jambo hilo. Kama kuna cho chote, yeye ataondoka aende mahali fulani kukuombea. Hiyo ni kweli. Lakini, loo, baadhi yao wako hai kabisa. Hilo ndilo ninalowazia, tunapaswa kuzika watu waliokufa. Hao waliokufa katika Kristo, tunawazika majini. Wakati mwingine tunazika watu wengi sana walio hai, uovu mwingi sana na ugomvi, na kuna mengi mno kanisani. Lakini hatuwezi kuwabagua hao, bali Mungu huwabagua. Yeye anawajua watu Wake. Yeye anawajua kondoo Wake. Yeye anajua kila sauti. Yeye anawajua watoto Wake. Yeye anajua ni nani anayeweza kumwita, anajua ni akina nani aliwachagua tangu zamani. Yeye anajua ni akina nani amewapa mambo haya, yale ambayo anajitambulisha kupitia kwayo. Jinsi Yeye … Mungu anaweza kuwaamini watoto Wake, juu ya yale ya kufanya, akijua kwamba wao watafanya kikamilifu kabisa.

36 Mnaamini Mungu hufanya hivyo? Mbona, Shetani alimwambia—Ayubu siku moja … akamwambia Mungu siku moja, "Naam, unaye mtumishi."

Mungu akasema, "Hakuna mtu duniani aliye kama yeye. Yeye ni mtu mkamilifu." NinaAlikuwa na imani na yeye.

Shetani akasema, "Loo, ndiyo, kila kitu kwake ni raha. Hebu nimchukue kwa kitambo kidogo na nitamfanya akukufuru usoni Mwako."

Yeye akasema, "Yeye yuko mikononi mwako, bali usiutwae uhai wake." Unaona? Naye alifanya kila kitu isipokuwa kuutwaa uhai wake.

Lakini, loo, Ayubu, badala ya … alifanya nini? Je! yeye alimkufuru Mungu wakati Mungu alipowachukua watoto wake, wakati alipomtendea mambo haya yote mabaya, na kila kitu? Ayubu hakuhoji. Alianguka kifudifudi na kuabudu, haleluya, kasema, "Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe!" Haya basi.

Mungu alijua alivyomwamini Ayubu. Mungu anajua kiasi gani anaweza kukuamini wewe. Yeye anajua ni kiasi gani anaweza kuniamini. Lakini kile tunachozungumzia sasa ni kumweka huyu mwana mahali pake.

37 Sasa, wakati Biblia … Wakati vita vitakapokwisha kabisa, wakati kila kitu kimemalizika, basi ni jambo gani tutatenda baadaye? Tutafanya nini baada ya vita kwisha? Je! Mlijua tutakalofanya? Tunakutana na Melkizedeki. Hebu tufungue Mathayo 16:16, upesi sana, tuone kama hilo ni kweli au la. Mathayo Mtakatifu, sura ya 16 na aya ya 16. Nina hakika kabisa kwamba hapo ndipo, Mathayo 16:16. Mathayo kumi na sita- … La, nimekosea, haiweza kuwa karibu hivyo. 26:26. Loo, 16 hapa, Yeye anazungumza na Simoni Petro; samahani, sikumaanisha kusema hivyo. 26:26, maana ni Meza ya Bwana tu, hapo ndipo ninapotaka kupakufikia. Mathayo, sura ya 26 na aya ya 26. Sasa tumepapata, haya basi, kwenye chakula cha mwisho.

> *Nao walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu.*
>
> *Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki;*
>
> *Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ajili ya ondoleo la dhambi* (d-h-a-m-b-i, dhambi, Wakristo wanaotenda mambo mabaya).

Vema, "Lakini—lakini …" Sikilizeni, aya ya 29.

> *… nawaambieni, sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.*

Ati nini? Jambo lile lile Melkizedeki alilofanya baada ya Ibrahimu kupata mahali pake. Akawaweka watu wake katika utaratibu, na akashinda vita, naye akarudi nyumbani, naye Melkizedeki akaja na mkate na divai. Baada ya vita kumalizika, ndipo tutakula Karamu ya Arusi pamoja na Bwana Yesu katika ulimwengu mpya. Loo, Jina la Bwana libarikiwe. Vema.

38 "Siri za mapenzi Yake, sawasawa na uradhi Wake," turudi sasa tena katika Waefeso, 9, "aliokusudia katikai Yake huyo."

*Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu …*

Na kumbukeni jambo hilo, tulilipitia tu hivi punde. Waefeso, sura ya 1, aya ya 10.

*Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu …*

Sasa, tulijifunza kwamba madaraka ya wakati mkamilifu ni kungojea nini? Utimilifu wa wakati wote, wakati ambapo dhambi itakoma, wakati ambapo mauti yatakoma, wakati ambapo magonjwa yatakoma, wakati ambapo dhambi itakoma, wakati ambapo upotovu wote (mambo hayo mapotovu, ambayo ibilisi ameyapotosa), yatakwisha, wakati majira yenyewe yatakwisha. Angalia.

*Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumuisha … vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia; Naam, katika yeye huyo:*

"Kuvijumuisha vitu vyote kwa njia ya Kristo." Kama nilivyosema asubuhi ya leo, vito vyote vidogo tunavyoona, mambo haya madogo yaliyo muhimu, unaweza kuyafafanua katika Mwanzo, unaweza kuyafafanua katika Kutoka, unaweza kuyafafanua katika Mambo ya Walawi, na kuyaleta kote, na katika Ufunuo yataishia kuwa Yesu. Mchukue Yusufu, mchukue Ibrahimu, mchukue Isaka, mchukue Yakobo, mchukue Daudi, kichukue chochote kimoja cha vito hivyo, hao watu wa Mungu, na uone kama humwoni Yesu Kristo akionyeshwa katika kila mmoja wao. "Apate kuvijumuisha vitu vyote katika Mtu moja, Kristo Yesu."

39 Sasa, mbele kidogo sasa, sasa hiyo aya ya 11.

*Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, …*

Loo, "urithi." Mtu fulani hana budi kukuachia kitu fulani, upate kukirithi. Je, hilo ni kweli? Urithi! Tuna urithi gani? Mimi nilikuwa na urithi gani? Sikuwa na wowote. Lakini Mungu aliniachia urithi wakati alipoliweka jina langu katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Loo, unasema, "Sasa, ngoja kidogo, ndugu, Yesu alifanya hivyo wakati alipokufa kwa ajili yako." La, Yeye kamwe hakufanya hivyo. Yesu alikuja kununua huo urithi kwa ajili yangu. Soma ile inayofuata … inayofuata papo hapo.

*Na ndani yake sisi nasi tulifanywa* kama … *tumefanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake;*

40 Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama tulivyolieleza kote katika somo, ninyi watu, jinsi tulivyoona kwamba Mungu aliishi peke Yake, jinsi ambavyo katika Yeye mlikuwemo na upendo. Ndani Yake mlikuwwemo kuwa Mungu; hakukuweko na kitu cha kumwabudu. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Baba; kulikuwako … Yeye alikuwa peke Yake. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Mwokozi; hakukuwa na kilichopotea. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Mponyaji. Hizo ni sifa Zake. Hapakuwepo na kitu hapo. Kwa hiyo Yeye Mwenyewe, shauri la mapenzi Yake Mwenyewe lilitoa mambo haya, ili kwamba katika Mtu huyu mmoja, Kristo Yesu, avikusanye vitu vyote pamoja tena. Loo! "Jicho halijaona, sikio halija …" Si ajabu ni jambo la ajabu!

41 Angalia, "ametuchagua tangu awali tupate huu urithi." Kama mimi nina haki ya kurithi kitu fulani, kama Mungu anabisha hodi moyoni mwangu na kusema, "William Branham, nilikuita muda mrefu uliopita, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuihubiri Injili," ninao urithi, urithi wa Uzima wa Milele. Sasa, Mungu alimtuma Yesu kuufanya urithi huo kuwa halisi kwangu, kwa sababu hakuna kitu ningeweza kufanya ili—ili kuurithi. Uikuwa mtupu, ulikuwa halali, nisingewe kufanya lolote. Lakini katika utimilifu wa wakati Mungu alimtuma, katika wakati Wake Mwenyewe uliofaa, Yesu aliye Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Damu Yake ilimwagika kusudi nipate kwenda kwenye urithi wangu. Kuwa nini, urithi gani? Uana, kuwa mwana wa Mungu.

42 Na sasa Hii linaweza kuwasonga roho nusura mfe. Lakini je! Mlijua ya kwamba watu ambao ni wana wa Mungu ni miungu wadogo? Ni wangapi waliopata kujua jambo hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alisema hivyo? Biblia, Yesu alisema, "Je! Torati yenu haikusema, yenyewe, ya kwamba ninyi ni 'miungu'? Na kama mkiwaita miungu …" Ambapo, Mungu alisema katika Mwanzo 2 kwamba wao walikuwa ni miungu, kwa sababu walikuwa hivyo, walikuwa na utawala mkamilifu juu ya milki ya ulimwengu. Alimpa utawala juu ya vitu vyote. Naye akapoteza uungu wake, akapoteza uwana wake, akapoteza milki yake, na Shetani akaichukua. Lakini, ndugu, tunangojea madhihirisho ya wana wa Mungu watakaorudi na kuimiliki tena. Tunangojea utimilifu wa wakati, wakati piramidi itakapofikia kileleni, wakati utimilifu wa wana wa Mungu utadhihirishwa, wakati nguvu za Mungu zitakapotembea (haleluya) na kumnyang'anya

Shetani kila nguvu aliyo nayo. Naam, bwana, ni mali yake.

43 Yeye ni Logos iliyotoka kwa Mungu, hiyo ni kweli, iliyokuwa Mwana wa Mungu. Kisha akamfanya mtu mungu aliye mdogo. Naye akasema, "Kama waliwaita hao waliojiliwa na Neno la Mungu liliwajia, hao manabii, kama waliwaita 'miungu' hao waliojiliwa na Neno la Mungu …" Na Mungu alisema hivyo, Yeye Mwenyewe, kwamba walikuwa miungu. Yeye alimwambia Musa, "Nilikufanya wewe mungu, na kumfanya Haruni nabii wako." Amina. Whiu! Huenda nikafanya kama kichaa wa kidini, bali sivyo nilivyo. Loo, wakati macho yako yanapoweza kufunguka na kuona mambo hayo. Vema. Yeye alimfanya mwanadamu mungu, mungu katika milki yake. Na milki yake inaenea kutoka bahari hata bahari, kutoka pwani hadi pwani; yeye ana mamlaka juu yake.

Na wakati Yesu alipokuja, akiwa ndiye yule Mungu Mmoja asiye na dhambi, Yeye alilithibitisha jambo hilo. Pepo zilipovuma, Yeye alisema, "Amani, tulia!" Amina. Na wakati mti, Yeye alisema, "Mtu asile kutoka kwako."

"Amin, nawaambia, ninyi mlio miungu midogo, mkiuambia mlima huu, 'ng'oka,' na msitilie shaka mioyoni mwenu, bali mwamini ya kwamba yale mliyosema yatatimia, mnaweza kupata yale mliyosema."

44 Rudini moja kwa moja kwenye Mwanzo, kwenye ile ya asili, ni nini? Sasa ulimwengu na viumbe vinaugua, vinalia, kila kitu kinasonga mbele. Nini? Kwa ajili ya madhihirisha ya wana wa Mungu, wakati wana wa kweli, wana waliozaliwa, wana waliojazwa watanena na neno lao linaungwa mkono. Ninaamini tuko kwenye mpaka wake sasa hivi. Naam, bwana. Uuambie mlima huu, na iwe hivyo.

"Ndugu, na—natamani *ninii*, jambo fulani lifanywe. Mimi ni muumini katika Yesu Kristo."

"Nakupa wewe katika Jina la Bwana Yesu Kristo." Amina. Huo hapo udhihirisho.

"Loo, ndugu, mimea yangu inakauka kule. Sijapata mvua yoyote."

"Nitakutumia mvua, katika Jina la Bwana." Hapo itakuja. Loo, kungojea, kuugua, viumbe vyote vikingojea kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu. Mungu aliliamuru hapo mwanzo. Alimpa mwanadamu hiyo milki.

45 Alimpa Yesu Kristo, naye Yesu akatoa kaw Jina Lake, pamoja na uhakikisho huu, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu nami nitalifanya." Loo, Ndugu Palmer! Kungoja kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, mahali pale, lile kanisa!

Kama nilivyosema, Kitabu cha Waefeso ni Kitabu cha Yoshua, na Yoshua akiwaweka watu mahali pao. Sasa, kama wasingetulia, naye amweke Efraimu hapa, na katika ardhi ya Manase, na *huyu* angerudi akigombana na kufanya ghasia, watapigaje hatua? Mmoja anaposema, "Mimi ni Mbatisti, mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mpentekoste, mimi ni wa Umoja, mimi ni wa uwili, mimi ni *Fulani*."

Utafanyaje jambo hilo? Simama kimya! Mungu anataka kuliweka Kanisa Lake, wana na binti za Mungu. Mungu, nipe kuishi nipate kuliona jambo hilo, ndilo ombi langu. Limekaribia sana hata karibu naweza tu kuligusa kwa mikono yangu, inavyoonekana. Liko papo hapo. Hilo ndilo nimetamani kuona, nikingojea wakati nitakapotembea barabarani; pale amelala kiwete, tangu tumboni mwa mama yake, "Sina fedha wala dhahabu." Loo!

46 Unafikiri kansa ni kitu? Biblia ilisema unakuja wakati ambapo watu wataoza wakali katika miili yao, nao nderi watakula mizoga yao kabla hata hawajafa. Kansa ni maumivu ya jino ukilinganisha na yale yanayokuja. Lakini, kumbukeni, kitu hicho cha kutisha kilikatazwa katika siku hiyo kuwagusa hao waliokuwa na Muhuri wa Mungu. Hilo ndilo tunaloshindania sasa, kuingia ndani na kuwekwa mahali petu katika Ufalme wa Mungu kabla mapigo haya ya kutisha hayajaanza. Loo, ni jambo zuri jinsi gani! Muda wa wakati, utimilifu wa wakati, ule urithi.

*Na ndani yake sisi nasi* pia … *tulifanywa … urithi, huku tukichaguliwa tangu awali* …

47 Tulipewa urithi wetu vipi, kwa njia gani? Kuchaguliwa tangu awali. Kuchaguliwa tangu awali ni kujua tangu zamani. Mungu alijuaje kwamba angekuaminisha kuwa mhubiri? Kujua Kwake tangu zamani. "Si kwa uweza wa yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, ama yeye … Ni Mungu mwenye kurehemu." Hiyo ni kweli, kuchagua tangu zamani. Yeye alijua kilichokuwa ndani yako. Yeye alijua kilichokuwa ndani yako kabla hata hujaja duniani. Yeye alijua kilichokuwa ndani yako kabla hakujakuwako na dunia ambamo ungeishi. Huyo—huyo ni Yeye. Huyo ni Mungu asiye na kikomo, yule asiye na kikomo. Sisi tuna kikomo, tunaweza tu kuwaza yaliyo na kikomo.

48 Yameniwia mengi tangu jambo hilo ndilo liliponipata. Sijui. Ninapowazia ya kule, niliposimama kule muda huo mfupi wa furahatele , na nikawazia, "Hakuna kesho." Hakukuwako na jana, hakuna magonjwa, hakuna huzuni. Hakuna furaha kidogo, kishai furaha tele; ni furaha tupu. Loo, jamani! Loo, niliposimama pale na kusema, "Ni kitu gani hiki?"

Sauti hiyo ilisema, "Huu ni upendo mkamilifu, na kila kitu ulichowahi kukipenda na kila kitu kilichowahi kukupenda kiko hapa pamoja nawe sasa."

"Na utatukabidhi kwa Bwana Yesu atakapokuja, kama kumbukumbu ya huduma yako." Niliwaona hao wanawake warembo wakiwa wamesimama pale, wote wakinishika na kupaza sauti, "Ndugu yangu wa thamani, mdugu mpenzi!" Niliwaona hao watu na nywele hizo za matimutimu zilizozunguka shingo zao hapa, wakikimbia, wakinikumbatia na kusema, "Ndugu yetu mpenzi!"

Ndipo nikawaza, "Hii inamaanisha nini?"

Yeye akasema, "Hao ni watu wako."

Nikasema, "Ati watu wangu? Hakuwezi kuwepo na akina Branham wengi namna hiyo, hawa ni mamilioni."

Yeye akasema, "Hao ni waongofu wako!" Haleluya. "Hao ni waongofu wako. Hao ndio ambao …" Kasema, "Unamwona yule anayesimama pale?" Mwanamke mrembo sana niliyepata kumwona. Kasema, "Alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Mungu. Si ajabu analia, 'Ndugu yangu mpenzi.'" Kasema, "Hatazeeka tena kamwe. Amepita hayo. Yeye yuko katika fahari ya ujana. Yeye amesimama hapa. Hawezi kunywa maji baridi, hana haja nayo. Hawezi kujilaza chini na kulala usingizi, maana yeye hachoki. Hakuna kesho, hakuna jana, wala chochote. Tuko katika Umilele sasa. Lakini siku moja yenye utukufu Mwana wa Mungu atakuja, nawe utahukumiwa kulingana na Neno ulilowahubiria." Loo, ndugu!

Nikasema, "Itabidi Paulo alete kundi lake?"

"Naam, bwana."

Nikasema, "Nilihubiri Hilo hasa tu kama vile Paulo alivyosema. Kamwe sikuepa, sikuingilia kamwe kanuni yoyote ya imani ya kanisa ama cho chote kile. Nilidumu vile vile."

Ndipo hao wote wakapaza sauti kwa pamoja, "Tunajua hilo! Tunapumzika kwa uhakika." Kasema, "Wewe utatukabidhi Kwake, na ndipo sote tutarudi duniani tena, tukaishi milele." Loo, jamani!

49 Mara nikaanza kujirudia. Nikaangalia, nimelala pale kitandani, na nikaona mwili wangu mzee hapa ukizeeka na kukunjamana, na umejikunyata na—na umejaa magonjwa na mateso, nami nikaona mikono yangu nyuma ya kichwa changu, nami nikawaza, "Loo, itanibidi kurudi katika kile kitu tena?"

Nami nikaendelea kuisikia Sauti hiyo, "Endelea kukaza mwendo! Endeleeni kusonga mbele!"

Nikasema, "Bwana, daima nimeamini uponyaji wa Kiungu, nitaendelea kuamini hilo. Lakini nitajitahidi sana kwa ajili ya hizo nafsi, hivyo basi nisaidie. Nitakuwa na wengi sana kule nita- … Jalia niishi, Bwana, nami nitaingiza milioni nyingine mle, iwapo utaniruhusu tu niishi."

50 Sijali ni wa rangi gani, ni wa imani gani, ni wa taifa gani, wao ni nini, wote ni mmoja wanapofika kule, na mipaka hiyo imepita. Loo, naweza kuwaona hao wanawake, warembo sana; sijapata kuona … ilikuwa chini, nywele ndefu zilizoning'inia kushuka chini sana mgongoni mwao. Sketi ndefu sana mpaka chini. Hawakuvaa viatu. Nikawaona hao wanaume wenye nywele za matimutimu zilizofika shingoni mwao, nywele nyekundu, nywele nyeusi, na rangi zote mbalimbali. Nao walikuwa wakinikumbatia kwa mikono yao. Niliweza kuwahisi. Nilihisi mikono yao. Mungu ndiye Hakimu wangu, na Kitabu hiki kitakatifu kilichofunguliwa. Niliweza kuwahisi kama vile tu ninavyoihisi mikono yangu kwenye uso wangu. Walikuwa wakinikumbatia kwa mikono yao, hakuna hisi ya wanawake kama ambavyo ingelikuwa sasa. Sijali wewe ni mtakatifu jinsi gani, wewe ni nani, wewe ni mhubiri wa aina gani, kasisi ama chochote unachoweza kuwa, hakuna mwanamume anayeweza kumruhusu mwanamke amkumbatie, bila kupata misisimko ya kibinadamu. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini, ndugu, unapovuka kati ya hapa na huko ng'ambo, sivyo ilivyo kule. Loo, jamani! Ni ninii sana … Loo, kuna … Haiwezekani. Yote ni upendo. Kila kitu ni halisi ndugu na kila kitu ni halisi dada. Hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna wivu, hakuna kitu chochote, hakuna kinachoweza kuingia pale. Ni ukamilifu tu. Hicho ndicho ninachoshindania. Hicho ndicho ninachoweka kwa ajili yake.

51 Nikasema, "Ee Bwana, hiyo ndiyo sababu niko hapa kanisani, nikijaribu kuliweka kanisa katika utaratibu." Nikikuambia ninyi, ndugu na dada, kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuingia pale, hicho ni upendo mkamilifu. Si kwa sababu wewe ni mwaminifu kwa Maskani ya Branham, ama kanisa la Kimethodisti au kanisa la Kibaptisti. Hayo ni sawa, mnapaswa kuwa hivyo. Lakini, loo, enyi marafiki, inawapasa … Si kwa sababu ulinena kwa lugha, ukacheza katika Roho, kwa sababu umetoa pepo ama kuhamisha milima kwa imani. Hayo yote ni sawa, kwa kuwa hayo ni sawa, lakini hata hivyo isipokuwa huo upendo mkamilifu halisi umo mle ndani. Hapo ndipo palipokuwa na upendo mkamilifu. Na hicho ndicho kitu pekee kitakachokuingiza mle. Hicho ndicho kitu pekee kinachoweza kudumu pale, ndicho kitu pekee kilichokuwepo, pale. Lo jamani! Ni kufanywa wana wenye mamlaka. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

52 Sasa, hebu tuharakishe, hebu tuimalize hii sura moja, hata hivyo, ikiwezekana, katika dakika kumi zinazofuata.

> *Tumefanywa urithi* … (Tunarithi nini? Uzima wa Milele) … *huku tukichaguliwa tangu awali* …

Vipi? Je! Kila mtu anaelewa jambo hilo? Je! Wewe ulimwita Mungu? La, Mungu ndiye aliyekuita. Watu wengine husema, "Loo, nilimtafuta tu Mungu, na kumtafuta Mungu."

Hukufanya hivyo. Hakuna mtu aliyewahi kumtafuta Mungu. Ni Mungu akimtafuta mtu. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Unaona, ni tabia ya mwanadamu kumkimbia Mungu. Nawe unasema sasa …

Hiyo, hiyo ndiyo inayonitatiza, hata hivyo, kuwahubiria ninyi watu; msibakie katika hali ile ile ambayo mmekuwa mkiingia, badilikeni sasa! Nisikilizeni ninaposema jambo hili , BWANA ASEMA HIVI. Sijawahi kujiita mwneyewe hivi, sivyo nilivyo. Lakini ninyi mnaniita mimi nabii wenu, ama nabii. Ulimwengu unaamini hivyo, ulimwengu kote, mamilioni na mamilioni na mamilioni ya watu. Nimenena uso kwa uso na kwa njia nyingine na watu milioni kumi ama—kumi au kumi na mbili, au zaidi, nikizungumza uso kwa uso. Nimeona maono maelfu kumi na ishara na maajabu, wala hakuna hata moja lililopata kushindwa. Na hiyo ni kweli. Yeye ameniambia awali mambo ambayo kamwe hayakushindwa kutukia kikamilifu. Nitamleta mtu yeyote kwenye mashindani juu ya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Mimi sidai kuwa nabii, bali ninyi nisikilizeni mimi.

53 BWANA ASEMA HIVI, itahitaji upendo mkamilifu kukuweka mahali pale, kwa kuwa huo tu ndio ulikuwa kule. Si hoja ni fedha ngapi, una madhihirisho mangapi ya kidini, ni matendo mangapi mema uliyofanya ama lo lote ulilofanya, hilo halitafaa kitu kwenye siku ile. Itahitaji upendo mkamilifu. Kwa hiyo lo lote ufanyalo, weka kando kila kitu kingine mpaka umekwishajazwa sana tu na upendo wa Mungu hata unaweza kuwapenda wale wanaokuchukia.

Niko tu kama nilivyosema asubuhi ya leo, nilifanywa, utu wangu wote ni neema. Watu wengi husema, "Sasa, wewe nikune mgongo wangu nami nitaukuna wako. Naam, unanifanyia jambo fulani nami nitakufanyia jambo fulani." Hiyo si neema. Neema ni, kama mgongo wako unakuwasha, nitaukuna hata hivyo, kama utaukuna wangu au la; ukinipiga kofi usoni, na kusema "mgongo wangu unahitaji kuwashwa, au, unahitaji kukunwa," nitaukuna. Unaona? Hivyo ndivyo ilivyo, fanya jambo fulani. Siamini katika matendo. Ninaamini ya kwamba matendo ni upendo. Matendo ni—matendo ni udhihirisho ya kwamba neema imekwishakuwako. Mimi siishi mwaminifu kwa mke wangu kwa sababu naamini atanitaliki kama nisingekuwa mwaminifu, naishi mwaminifu kwake kwa sababu nampenda.

54 Mimi sihubiri Injili ati kwa sababu nafikiri ningeenda kuzimu kama sikuihubiri, ninahubiri Injili kwa sababu nampenda. Hakika. Mnafikiri ningevuka hizo bahari zenye tufani, na hizo ndege zikipiga mbizi na kupanda juu, na radi ikimulika kila upande, na—na kila kitu kingine, na karibu dakika yo yote … na kila mtu akipiga mayowe, na "Salamu Mariamu" zikifululiza kila mahali kwenye hiyo ndege, na kila kitu? Hao watu wakisukwasukwa katika hiyo mikanda ya usalama, na rubani akisema, "Tunayo mafuta ya kutosha tu kwa dakika kumi na tano zaidi, sijui tuko wapi." Mnafikiri ningefanya hivyo kwa—kwa ajili ya kujifurahisha tu? A-ha! Mnafikiri ningerudi kule msituni ambako iliwabidi askari wa Kijerumani kunizungushia mikono yao namna *hii* kila usiku na kuniingiza na kunitoa mkutanoni, mpaka Roho Mtakatifu alipoanza kufanya miujiza? Wakomunisti wamekaa na darubini zao za usiku, wanipige risasi umbali wa maili moja. Mnafikiri ningefanya hivyo kwa ajili ya kujifurahisha tu? Kwa sababu kitu fulani ndani yangu kinapenda; hao ni wanadamu ambao Kristo aliwafia. Paulo alisema, "Mimi siko tu tayari kwenda Yerusalemu, bali ninaenda kule kusulubiwa. Napanda kwenda kule nipate kufa. Ninaenda huko nikafe kwa ajili ya kusudi la Bwana." Ni kitu fulani, upendo ambao unakushurutisha, unaokufanya. Hiyo ni kweli kabisa.

55 Kama ningehubiri Injili kwa ajili ya fedha, kama ingekuwa hivyo, nisingekuwa na deni la dola elfu ishirini usiku wa leo, nisingekuwa katika deni namna hiyo. La, bwana. Kwa sababu ningehifadhi baadhi ya —baadhi ya mamilioni niliyopewa. Mtu mmoja, mtu mmoja alimtuma kachero wa F.B.I. na hundi ya dola milioni moja na mia tano elfu. Nami nikasema, "Irudishe." Si kwa ajili ya fedha! Si fedha. Sihubiri Injili kwa kwa ajili ya fedha. Si kwa ajili ya hizo!

Ni kwa sababu ya upendo. Jambo ninalotaka kufanya, ni, nitakapovuka pumzi hiyo ya mwisho kule ng'ambo, jambo ambalo laweza kutukia mnamo dakika tano kutokea sasa, huenda ikawa ni masaa mawili kutokea sasa, huenda ikawa ni miaka hamsini tangu sasa, sijui itakuwa lini. Lakini wakati huo utakapowadia, nami niwasili kule, nataka kukuona katika fahari ya ujana, ukipiga mbio, ukipaza sauti, "Ndugu yangu mpenzi! Ndugu yangu!" Hilo ndilo lililoko moyoni mwangu. Hiyo ndiyo sababu yake. Sijaribu kutokubaliana nanyi kusudi niwe—niwe tofauti, bali ninajaribu kuwaweka kwenye njia ambayo sahihi. Hiyo ndiyo njia ya kuingia. Si kanisa lako, si dhehebu lako, bali kuzaliwa kwako katika Kristo. Loo, jamani. Whiu!

> *Na ndani yake … nasi tulifanywa … urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.*

56 Sikilizeni. Tutafunga katika dakika chache. Sikilizeni kwa makini sasa kabla hatujafunga.

*Nasi katika huyo tupate kuwa sifa za utukufu wake, sisi tuliotangulia kumwekea … Kristo tumaini letu.*

*Nanyi pia katika huyo* mmekwishamtumaini, …

Angalia jambo hili sasa, kwa makini. Vaeni makoti yenu, makoti ya Injili. Fungueni masikio yenu wazi, mkasikilize kwa makini. Niko kwenye aya ya 13.

*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia …*

"Imani huja kwa …" [Kusanyiko linasema, "Kusikia." — Mh.] "kusikia …" ["Neno."] "Neno la …" ["Mungu."]

*… mmekwisha kulisikia Neno la kweli, …*

Kweli ni nini? Neno la Mungu. Je, hilo ni kweli? Yohana 17:17, ninyi mnayaandika Maandiko, Yesu alisema, "Watakase, Baba, kwa ile Kweli. Neno Lako ni Kweli."

… Baada ya ninyi kuisikia ile *kweli, Injili ya wokovu wenu: …*

57 Ni wokovu gani aliokuwa anajaribu kuwaambia? Kuchaguliwa tangu awali kabla ya kuwekwa misingi ya dunia (Sivyo?), wapate kufanywa wana wenye mamlaka, waliochaguliwa tangu awali kwa ajili ya Uzima wa Milele. Sasa, baada ya ninyi kuingia katika Uzima wa Milele, mkiisha kuokolewa, kutakaswa, kujazwa na Roho Mtakatifu, ninyi ni wana. Sasa Mungu akitaka kukuweka mahali pako, loo, ili uweze kufanya kazi kwa ajili ya Ufalme Wake na utukufu Wake.

Hiyo ndiyo Injili. Mkiwa, kwanza, mnasikia Neno, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi." Kuziondoa dhambi zenu zote, mkiliitia Jina la Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya Nchi ya ahadi. Ahadi hiyo ni kwa kila msafiri anayesafiri. Kama uliondoka nyumbani mwako usiku huu, ukiwa mwenye dhambi, ukisema, "Nitaenda kwenye Maskani ya Branham," Mungu anakupa nafasi usiku huu. Kuna kitu kimoja kilichokaa kati yako na Nchi ya ahadi. Nchi ya ahadi ni nini? Roho Mtakatifu. Kilichokuwa kati ya Yoshua na nchi ya ahadi kilikuwa ni Yordani. Sahihi kabisa.

58 Musa, akiwa ni mfano wa Kristo, aliwaongoza wale wana hadi kwenye nchi ya ahadi, halafu Musa hakuwaingiza hao wana katika nchi ya ahadi. Yoshua ndiye aliyewaingiza hao watu na kuigawanya ile nchi. Yesu alilipa ile gharama, akawaongoza hadi kwenye Roho Mtakatifu. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu akashuka Naye akaja na kuliweka kanisa katika utaratibu, kila mtu, akimjaza na Uwepo wa Utu Wake. Mnaona ninalomaanisha? Yote katika Kristo Yesu, jinsi Mungu alivyochagua jambo hili tangu awali kwa ajili ya kuitwa kwa Injili hii!

Paulo, Wagalatia 1:8, alisema, "Kama Malaika akija akihubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe." Ile Kweli, Injili. Sasa sikilizeni kwa makini tunapoendelea kusoma, kumalizia hii aya.

*… Habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha …* (sikilizeni kwa makini) *… tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri kwa Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu,*

59 Katika siku za mwisho, Biblia ilisema, sasa angalia, katika siku za mwisho kutakuwa na tabaka mbili za watu. Moja litakuwa na Muhuri wa Mungu, hilo lingine alama ya mnyama. Je, hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua hivyo? Vema, kama Muhuri wa Mungu ni Muhuri wa … Kama Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu, basi bila Roho Mtakatifu ni alama ya mnyama. Na Biblia ilisema ya kwamba hizo roho mbili zingefanana sana ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Haitafanya hivyo kamwe, kwa sababu hao walichaguliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele. Unaona?

60 Kanisa likiendelea, kama tu kujua kuna wanawali kumi waliotoka wakaenda kumlaki Bwana, wote wametakaswa, wote watakatifu, kila mmoja wao ametakaswa. Watano walikuwa wazembe na kuacha taa zao zizimike. Watano walikuwa na mafuta katika taa zao. "Na tazama, Bwana Arusi yuaja!" Na wale watano waliokuwa na mafuta katika taa zao wakaingia kwenye ile Karamu ya Arusi. Na hao wengine waliachwa nje ambako kulikuwa na kilio na kuomboleza na kusaga meno. Iweni tayari, kwa maana hamjui ni dakika gani Bwana atakapokuja. Kuweni … Mafuta yanawakilisha nini katika Biblia? Roho Mtakatifu.

61 Sasa kwenu leo, ninyi ndugu wa Seventh-day Adventist mliosema kwamba siku ya saba ndiyo Muhuri wa Mungu, toeni Andiko moja kuthibitisha jambo hilo. Biblia ilisema kwamba Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Angalieni jambo hili. "Ambalo …" Angalieni kwenye aya ya 13 sasa.

*… tena ninyi mmekwisha kumwamini yeye,* nanyi *kutiwa muhuri na* yule—*na Roho yule wa ahadi aliye Matakatifu.*

Fungueni Waefeso 4:30, naamini hapo ndipo. Tuone kama hatutapata 4:30, tuone kama hilo silo lile lile. Waefeso, sura ya 4 na aya ya 30. Naam, hii hapa, 4:30.

*Wala msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri* mpaka *siku ya ukombozi.*

62 Muda gani? Unapompokea Roho Mtakatifu kweli kweli, Yeye atakudumisha kirefu kiasi gani? Mpaka ufufuo unaofuata, mpaka bibi atakapokuudhi, mpaka tajiri yako atakapokugombeza? Hata siku ya ukombozi wako! Haleluya!

Ukiisha kufa, ukiishavuka ukaingia katika Nchi hiyo, ambapo unasimama kule pamoja na wapenzi wako, ungali utakuwa umejazwa na Roho Mtakatifu. Maandiko! Uko tu jinsi ulivyo sasa, isipokuwa una … umeingia katika mwili mwingine. Ulibadilisha tu makao. Huu ulizeeka, usingeweza kuutengeneza tena, pao zimeoza. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo unakiachia tu hicho kitu cha kale na kuacha kiendelee kuoza, kisha unaingia kwenye ulio mpya. Hiyo ni kweli? "Kwa maana maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja inayongoja."

63 Mnakumbuka hivi majuzi, tukipitia hayo? Wakati mtoto mchanga anaumbwa katika tumbo la uzazi la mama, na misuli hii midogo inapigapiga na kurukaruka na kuendelea. Lakini mara tu mama anapomzaa mtoto mchanga na huyo mtoto mchanga anafika duniani, jambo la kwanza, kuna mwili wa kiroho kuupokea huo mwili mdogo wa maumbile ya asili. Labda daktari anampa … [Ndugu Branham anapiga makofi — Mh.] namna *hiyo*, ama kitu fulani cha kumtikisa, kisha "wha, wha, wha." Na mara anaingia kwenye titi la huyo mama litaenda, "um, um, um," akisogeza kichwa chake kidogo juu na chini kwenye titi la mama yake, kuifanya hiyo mishipa ya maziwa ilete maziwa.

Ndama mdogo, mara tu anapozaliwa na mama yake, atasimama kwa magoti yake madogo baada ya dakika chache. Atafanya nini? Atazunguka moja kwa moja upande wa nyuma, atamshikilia huyu mama, na kuanza kutikisa kichwa chake kidogo juu na chini namna hiyo, na kujipatia maziwa yake. Haleluya! Naam, bwana.

Wakati mwili huu wa kawaida unapoingia ndani ya mama, kuna mwili wa kiroho unaoungojea.

Na wakati mwili huu wa kawaida unapoangushwa ardhini, haleluya, kuna mmoja unaoungojea kule! Tunaondoka tu kutoka kwa mmoja kwenda kuingia kwa mwingine, tunabadilisha makao yetu. Huyu wenye kupatwa na mauti hauna budi uvae kutokufa, huu wa kiroho; huu uharibikao uvae wa kutokuharibika. Huu mwili wa kale, wenye makunyanzi, unaojikokota, na uliojikunyata, lakini hautabadilisha mwonekano wake hata kidogo, namaanisha utakapofika kule ng'ambo, bado utakuwa na roho yule yule.

64 Hebu niwapeni kitu kidogo kinachoonekana kama kinatatiza kwenu, bali ni Biblia, kisha nitawapa kimoja ambacho hakitawatatiza. Angalia jambo hili. Wakati mzee Sauli, yu—yue mfalme, maskini yu—yule mzee mhubiri mashuhuri wa kidhehebu kule chini wakati huo, mwajua, ambaye tokea kichwa hata mabega alikuwa mrefu kuliko hao wote, naye aliogopa, wao hawakujua kitu kuhusu yale ya Kimbinguni. Ilimlazimu Daudi kuja na kumwokoa mwana-kondoo kutoka kinywani mwa simba, akamwua Goliathi. Mwangalie. Alienda mbali sana na Mungu, akaanza kumchukia mhubiri huyu mtakatifu anayejiviringisha. Na badala ya kuwa upande wake, kujaribu kumsaidia, alikwenda kinyume naye. Kama hiyo si picha hasa, ile picha hasa. Akawa kinyume naye moja kwa moja!

65 Ni wangapi waliokuwa humu wakati nilipoondoka kwenye ziara yangu ya kwanza, kuhubiri, "Juu ya Daudi akimwua Goliathi," nilipoondoka? Wengi, baadhi, wachache wa hao watu wa zamani. Ninajitayarisha kuondoka tena juu ya jambo hili. Mnakumbuka kile, mliona hasa kilichotokea Jumapili iliyopita? Inasogea kuingia moja kwa moja katika kiwango kingine. Kampeni ya pili ya Daudi, kiwango cha pili cha huduma yake. Hiyo ni kweli kabisa. Ambapo, ndipo akawa mfalme wa Israeli. Angalia huduma sasa inaingia katika kiwango kikuu zaidi, inakuwa ya hali ya juu zaidi. Vivyo hivyo na Daudi. Naona jambo hili wakati anapokuja, Daudi, loo, wakati Mungu alipomfanya Daudi atoke huko na kumwua yule simba, tazama, na kumwua dubu, kisha kumwua Mfilisti. Sasa, ukaja wakati ambapo Mungu alimpa maskini kijana huyu roho mchafu juu ya mvulana huyu mzee. Na juu ya … Afanyeje? Amchukie Daudi. Nami naamini …

66 Sasa, kanda hizi. Sasa sikilizeni, ndugu, ninyi mlio kwenye kanda hizi, kama hamkubaliani nami, nisameheni. Unaona, nawapenda. Nitakutana nanyi huko ng'ambo hata hivyo, unaona, maana kama wewe ni mtu wa Mungu nitakutana nawe hata hivyo. Lakini, nataka kusema jambo hili, sababu yake ndiyo hii. Kwa sababu tu ya kwamba Sauli aliona ya kwamba Daudi alikuwa na kitu ambacho yeye mwenyewe hakuwa nacho. Ndipo ikatokea nini?

Maskini kijitu "chekundu," kilichoinama, Biblia ilisema alikuwa "mwekundu." Huyo hakuwa mtoto mzuri sana, "mwekundu" ni namna ya maskini jamaa mdogo aliyeinama. Naye akatoka akaenda kule, na Sauli, mbona, akajivika silaha za Sauli, nami nadhani ile ngao ilifika hadi miguuni mwake. Naye akasema, "Nivueni vitu hivi. Mimi—mimi nime …" Labda alimpa digrii ya udaktari, Ph.D. ama L.L.D., ama kitu fulani, mnajua. Jinsi alivyosema, "Sijui chochote juu ya kitu hicho, kwa sababu sijakithibitisha. Hebu nichukue hiki, kile ninachojua nafanya nacho." Naam, bwana. Akachukua kombeo.

67 Nao walimkasirisha Daudi kwa sababu hao mabinti, makanisa, makanisa yalikuwa yanaimba, "Sauli,

huenda aliua maelfu yake, bali Daudi aliua makumi elfu yake."

Ndipo akawa na wivu, "Ni upuuzi huo wa siku nyingiwa Jina la Yesu, hakuna kitu Kwake." Hiyo ni kweli. Na Mungu alimfanyia nini? Mungu alimtumia pepo mchafu, kumchukia Daudi, naye alimchukia Daudi bila sababu.

Daudi angeweza kumnyonga shingo mara kadha. Yeye angeweza, bali aliliachilia tu liende. Yeye kamwe hakusema kitu. Hakika angeweza kufanya hivyo. Alienda kule na kukata upindo wa koti lake, usiku mmoja, akarudi, kasema, "Angalia hapa, unaona!" Naam, bwana, angaliweza kufanya hivyo, bali alimwachilia tu. Yeye angiweza kulivunja kusanyiko lake na kuwatawanya, na kuanzisha shirika lake mwenyewe kama alitaka kufanya hivyo. Lakini yeye hakufanya hivyo, alimwacha tu Sauli aendelee. Akaacha Mungu apigane. Ndiyo, bwana.

68 Kwa hiyo alipotoka akaenda zake na kampeni ikaisha, na akaendelea, huyo pepo mchafu akampagaa hivi kwamba Sauli hakuwezakupata jibu kutoka kwa Mungu. Baada ya kitambo kidogo yeye … Roho wa Bwana alikuwa amemwacha. Naye mzee Samweli, yule waliyekuwa wamemkataa, yule ambaye kweli alikuwa ndiye Sauti ya Mungu kwao, yule ambaye aliyaambia kabla hata hawajataka kuenenda kama ulimwengu.

Kanisa linatakaje kuenenda kama ulimwengu? Kwa nini Pentekoste, Methodisti waliobatizwa, waliopata tukio la Roho Mtakatifu, na Baptisti, na Presbiteri wanataka kutenda kama ulimwengu? Kwa nini wanafanya hivyo? Mimi sijui. Si—hata siwezi kamwe kulielewa jambo hilo. Unasema, "Vema, inafurahisha sana kucheza karata, kujifurahisha kidogo tu, senti kidogo tu za kucheza karata," cho chote mnachoiita. Ni dhambi. Haikupasi kuwa na vitu hivyo nyumbani mwako. "Mbona, hakuna ubaya wa kunywa glasi moja ndogo tu ya bia. Tumekwishakunywa chache tu. Mimi na mke wangu hunywa chache alasiri." Na muda si muda unajua, watoto wako wana chache. Hakika ndivyo ilivyo.

69 Na ninyi wanawake, hum, ibilisi amewafanya tu … Hivyo ndivyo alivyofanya hapo mwanzo, naye hakika amewafanyia akina dada lengo. Yeye hufanya hivyo tu ili … maana anajua anachoweza kufanya. Anaweza kumdanganya mwanamke mara elfu moja haraka zaidi kuliko anavyoweza kumdanganya mwanamume. najua hilo linaumiza hisia zenu, lakini hiyo ni Kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo alivyofanya katika bustani ya Edeni. Anaweza kumfanya … Sasa, yeye alikuwa mwaminifu, alikuwa na moyo mweupe, bali alidanganywa. "Adamu hakudanganywa," Biblia ilisema. Mwanamume hakudanganywa, bali mwanamke alidanganywa. Kwa hiyo anaweza kumdanganya. Na hata hivyo wachungaji wataondoka moja kwa moja na kuweka wakfu wanawake kuwa wahubiri, na kuwaweka kule kutawala makusanyiko namna hiyo, na Biblia hii inalaani jambo hilo kutokea kwenye Mwanzo hadi Ufunuo. Unasema, "Vema, ni sawa. Ni sawa. Wao wana … Wanaweza kuhubiri sawasawa kama tu hao." Ninajua hiyo ni kweli.

70 Ni kama vile mtu mmoja aliyeanza kunena kwa lugha wakati mmoja, mimi niliendelea tu kuhubiri. Na nilipofika nje, mwanamke mmoja akamwambia mwanangu, kasema, "Nina ujumbe nitakaotoa kesho usiku," kasema, "wakati Baba yako atakapokuja jukwaani."

Kasema, "Vema, Bibiye, unamaanisha nini?"

Na usiku huo mambo yalipokuwa tayari, wakati nilipokuwa nikijiandaa kutoa wito wa madhabahuni, yule mwanamke akatengeneza nywele zake vizuri na kuvuta soksi zake na kila kitu, akajiandaa, akaruka juu katikati ya sakafu na kuanza kurukaruka, akanena kwa lugha na kutabiri. Niliendelea tu kuhubiri, nikafanya wito wangu wa madhabahuni. Nami sikuliheshimu jambo hilo hata kidogo, halikuwa sahihi. Kwa hiyo basi, vema, Biblia ilisema lisiheshimiwe, ilisema, "Roho wa manabii humtii nabii." Mungu yuko kwenye … Mungu akiwa ananena jukwaani, mwache anene. Paulo alisema, "Kama jambo fulani likifunuliwa kwa mtu mmoja, hebu na atulie mpaka huyo mwingine atakapomaliza." Hiyo ni kweli.

Sasa, basi nilipotokaka nje, hawa watu wakasema, kundi kubwa la watu, likasema, "Ulimhuzunisha Roho Mtakatifu usiku wa leo."

Nikasema, "Vipi? Nilifanyaje?"

Kasema, "Vema, wakati yule dada alipotoa ujumbe huo, haleluya, kasema hivyo."

"Mbona," nikasema, "nilikuwa nikihubiri. Yeye alikuwa nje ya utaratibu."

"Loo," kasema, "huo ulikuwa mpya moja kwa moja kutoka kwenye Kiti cha Enzi. Huo ulikuwa mpya zaidi kuliko lue ulilokuwa ukihubiri." A-ha!

71 Sasa, hilo linaonyesha tu ninii … hilo linaonyesha ama jambo hili, nami nalisema kwa heshima yenu, aidha ukichaa, ama aidha kutokuheshimu, ama mafundisho ya kijinga ambayo hayamjui Mungu zaidi ya sungura anavyojua kuhusu viatu vya theluji. Sasa, hilo, sisemi hilo liwe ta—tamshi ya kipumbavu, kwa sababu hapa si mahali pa kufanya mzaha. Lakini hilo—hilo ni kweli kabisa. Mtu ambaye angejua ya kwamba Mungu si mwanzilishi wa machafuko. Yeye ni wa amani. Hawaijui Biblia. Yote waliyojua jinsi ya

kufanya ni kurukaruka, kunena kwa lugha, kusema, "Nina Roho Mtakatifu. Haleluya!"

Nimesimama na kuona, huko Afrika, wachawi na kadhalika wakinena, wakiwemo elfu tano wao kwa wakati mmoja; wakirukaruka, damu ikiwa kote usoni mwao, wakinena kwa lugha, na kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu; wanamwita Ibilisi, na kunena kwa lugha.

72 Na hata hivyo kunena kwa lugha ni karama ya Mungu, lakini huo si uthibitisho usiokosea wa Roho Mtakatifu. Hebu niwaambie jambo hilo sasa. Ninaamini ya kwamba watakatifu wote waliovuviwa hunena kwa lugha. Ninaamini kwamba mtu wakati mwingine unapovuviwa sana na Mungu mpaka utanena kwa lugha. Ninaamini jambo hilo. Lakini siamini hiyo ni ishara yoyote kwamba una Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Ninaamini kuna wakati ambapo unakuwa na imani, huyo mtu, ungeondoka uende moja kwa moja na kumwekea mikono mtoto mdogo aliye na kansa, wakati wahubiri hamsini walikuwa wamemwombea, naye angeponywa kwa sababu huyo mama ana imani kwa ajili ya mtoto huyo. Mungu amempa hiyo, yeye ni mshiriki wa Mwili wa Kristo. Naam, bwana. Ninaamini jambo hilo. Nimeona jambo hilo likitendeka na ninajua hilo ni kweli. Lakini jambo lenyewe ni kwamba, ni kuliweka kanisa katika utaratibu, kuliweka katika utaratibu ili tuweze kufanya kazi.

73 Sasa hebu tumalizie aya hii iliyosalia hapa kabla hatujaondoka.

> … baada ya ninyi kupokea, *na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi aliye Mtakatifu.*

"Kutiwa muhuri!" Muhuri ni nini? Muhuri ni nini? Muhuri ni, jambo la kwanza inaloonyesha ni kazi ambayo imemalizika, kazi iliyomalizika. Jambo lingine inaloonyesha ni umiliki. Na jambo lingine inaloonyesha ni usalama, kuutunza.

Tuseme, kwa mfano, nilikuwa nikifanya kazi kwenye Shirika la Reli la Pennsylvania, nilikuwa nikifanya kazi kwenye njia ya reli pamoja na baba yangu. Tungeyapakia mabehewa. Nasi tungeyaleta hapa chini kwenye kampuni hii ya kupakia, tungepakia makopo, na tungeyaweka mengine juu *hapa* na mengine hapa chini, na mengine tuyaweke juu namna *hii*. Lakini kabla hilo behewa halijatiwa muhuri, mkaguzi alipitia pale, naye akalisukuma, akalipiga *hili* kumbo, akatikisa *lile*. "Ah! Limekataliwa! Yote yatavunjika vipande—vipande kabla hayajafika kule. Limekataliwa! Yatoeni. Rudieni tena." Mkaguzi alilikataa lile behewa.

74 Roho Mtakatifu ndiye Mkaguzi. Yeye anakutikisa kidogo, nawe unatatarika. Je! Unaamini Neno lote la Mungu? "Siamini upuuzi huo wa kale wa Jina la Yesu." Analikataa. Unatatarika, mnaona. "Siamini katika uponyaji wa Kiungu wala kitu kama hicho." Bado unatatarika. Yatoe. Unaamini Yesu Kristo ni yeye yule jana … "Vema, kwa namna fulani." Unatatarika. Lipige teke nje, unaona, bado haliko tayari. Ndio, bwana.

Ndugu, wakati liko tayari husema, "Amina!" Umepokea Roho Mtakatifu? "Amina!" Je! Kila kitu kimeishakamilishwa? "Amina." Basi Mkaguzi anafanya nini? Kila kitu kimepakiwa mle ndani vizuri na kukazwa, kimejaa Injili. Loo, kila Neno la Mungu ni zuri. Kila kitu ni kikamilifu. "Ninaamini kila Neno. Amina! Amina! Amina!" Je! Unaamini ya kwamba Mungu angali anaponya? "Amina." Unaamini Yesu ni yeye yule jana na hata milele? "Amina." Unaamini Roho Mtakatifu ni halisi tu kama alivyowahi kuwa? "Amina." Je! Unaamini Roho yule yule aliyeshuka juu ya Paulo hutushukia sisi? "Amina." Je! Unaamini anafanya mambo yale yale juu yetu aliyofanya juu yao? "Amina." Loo, loo, linaanza kukazika sasa. Unaona, linaanza kukazika sasa, tuko tayari kufunga mlango. Vema.

75 Ndipo mkaguzi anafunga mlango. Yeye anafanya nini? Yeye analitia muhuri juu yake. Ndipo anashuka chini hapa na kuchukua vitu kama koleo hizi ndogo, anashika kile kidude kidogo pale na kulitia muhuri. Usithubutu kuivunja. Kama hayo, hilo behewa, linaenda Boston, huwezi kuivunja. Ingekuwa ni adhabu ya kifungo kufungua huo muhuri hata litakapofika Boston. Na mtu aliye na mamlaka anaweza kufungua muhuri huo, na ni yeye peke yake. Hiyo ni kweli. Ni mali ya shirika *fulani* la reli. Ni muhuri wao. Ni uhakikisho wao ya kwamba behewa hili liko tayari, behewa hili liko tayari. Ni mali yao. Wasingeweza kuweka ile "B & O" kwenye "Pennsylvania." Huna budi kutiwa muhuri, na wakati linapotiwa muhuri.

76 Na wakati Mkristo amepakiwa Injili, amejazwa na wema wa Mungu, mambo yote mazuri ya Mungu yakikaa ndani yake, akiwa na moyo mweupe, akiwa tayari kufanya kazi, akiwa tayari kuwekwa mahali pake, kufanya lolote ambalo Roho Mtakatifu anamwambia afanye, amepita kutoka mautini kuingia Uzimani, ametakaswa mbali na mambo yote ya ulimwengu, akitembea katika Nuru jinsi Nuru inavyomjia, akisonga mbele, yeye yu tayari. Ndipo Mungu huufunga mlango wa ulimwengu nyuma yake, na kuupiga pamoja namna hiyo, na kumtia muhuri kwa Roho Mtakatifu wa ahadi. Haleluya! Kwa muda gani? Hadi kwenye kikomo. Usimwondoe nje hapa kwenye nji ya reli na kumfungua uone kama kila kitu kiko sawa tena. Ni sawa, mwache tu jinsi alivyo. Mkaguzi amekwishalikagua. Umetiwa muhuri kwa muda gani? Hata siku ya ukombozi wako. Huo ndio muda uliotiwa muhuri.

"Vema, unapokufa, basi, Ndugu Branham, vipi baada ya wewe kufa, ulisema ungali unao?" Unao milele. Uzima unaanzia wapi? Madhabahuni. Papo hapo unaona kivuli kidogo. Hicho ni kivuli, Muhuri wa Roho Mtakatifu. Basi ni kivuli cha vivuli vya vivuli, kama nilivyosema hivi majuzi. Lakini wakati unapokufa, unaendelea kupitia kwenye vivuli hivyo mpaka unapofikia kwenye unyevu, kutoka kwenye unyevu hadi

kwenye chemchemi ndogo inayotiririka, kutoka kwenye chemchemi hadi kwenye kijito, kutoka kwenye kijito hadi kwenye mto, kutoka mto hadi kwenye bahari, unaona, ya upendo wa Mungu. Wewe ni mtu yule yule tu.

77 Angalia hapa. Mzee Sauli, yule mzee maskini aliyerudi nyuma, hangeweza kumfikia Mungu, hata hivyo hakuwa amepotea. Hakika hakuwa amepotea. Yeye alikuwa nabii, bali alienda tu mbali na Mungu. Hiyo ndiyo sababu, ndugu, nilisema, "Hujapotea." Kwa hiyo basi kumbukeni, yeye alitoka tu nje ya mapenzi ya Mungu, kwa hiyo basi, jambo la kwanza unajua, yeye—yeye hangekubali. Sasa, labda nisingesema hilo. Vema, ninaendelea tu kwa ajili ya kusanyiko lenye furaha usiku wa leo. Kwa hiyo basi, unajua, na jambo la kwanza unajua, loo, jamani, ndipo ninii … Yeye alienda kwenye Urimu Thumimu.

Mnajua Urimu na Thumimu ilikuwa nini, ilikuwa ni kifuko cha kifuani, ile naivera ambayo—ambayo Haruni aliivaa. Nayo ilikuwa daima, Mungu daima amekuwa ni Mungu wa kimbinguni akijibu katika njia za kimbinguni. Na wakati nabii alipotabiri, na hizo nuru za kisiri hazikumulika kwenye hiyo Urimu Thumimu, alikuwa amekosea. Wakati mwotaji aliposimulia ndoto nayo haikumulika kwenye hiyo Urimu Thumimu, sijali ilionekana kuwa nzuri jinsi gani, ilikuwa ni makosa. Hiyo ni kweli.

78 Nami sijali una digrii ngapi hasa za juu daktari na dhehebu lako ni kubwa jinsi gani, unapotabiri ama kuhubiri, na si kulingana na Neno hili, umekosea, ndugu. Wewe ni … Hili ni Urimu na Thumimu ya Mungu. Unaposema haukuchaguliwa tangu awali kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, haitamulika, kwa sababu Biblia ilisema ulichaguliwa. Unaposema ya kwamba unapaswa kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," haimuliki, kwa sababu hakuna mtu katika Biblia aliyewahi kubatizwa namna hiyo. Ni katika Jina la Bwana Yesu tu. Haitamulika, kwa hiyo kuna kasoro mahali fulani.

79 Kwa hiyo Urimu na Thumimu haingemjibu mzee Sauli, na hata asingeweza kupata ndoto. Alikuwa amekengeuka mno mpaka asingeweza kupata ndoto. Kwa hiyo unajua alichofanya? Alishuka akaenda kwa yule mchawi, na huyu mchawi mzee, maskini daktari wa ibilisi kule chini, mchawi. Naye akasema, "Je! Waweza kuniagulia?"

Akasema, "Naam, lakini Sauli alisema angemwua kila mtu anayeagua."

Akasema, "Nitakulinda," huku amevalia kama mtumishi. Akasema, "Niagulie ukanipandishie kutoka kwenye ulimwengu wa wafu wale waliovuka ng'ambo ya pili." Sasa sikilizeni jambo hili. "Nipandishie roho ya nabii Samweli."

Naye akaingia ndani—akaague. Na, alipofanya hivyo, akaanguka kifudifudi, akasema, "Naona miungu ikipanda" Unaona, yeye alikuwa kafiri, "miungu," wawili ama watatu wa hao, kama vile Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, ama kitu kama hicho, mwajua. Akasema, akasema, "Naona miungu ikipanda."

Kasema, "Toa wasifu wake. Ni mfano wa nani? Anafanana na nani?"

Kasema, "Yeye ni mwembamba na ana vazi mabegani mwake." Hakuwa amebadilika, hata kidogo.

Akasema, "Ni Samweli. Mleteni humu chumbani, mlete hapa mbele yangu."

Na tazama wakati Samweli alipokuja mbele ya Sauli, alisema, "Mbona ukaniita, nawe umekuwa adui wa Mungu?" Na tazama. Yeye hakuwa tu yungali Samweli, alikuwa angali ana roho ya unabii. Semeni si kweli, hebu mtu yeyote aseme ni kosa. Ni Kweli! Yeye alikuwa angali ni nabii. Kwa kuwa alisema, alitabiri na kusema, "Kesho utashindwa vitani, nawe pamoja na wanao mtaangamizwa, na wakati kama huu kesho usiku utakuwa pamoja nami." Je, hilo ni kweli? Yeye alikuwa angali ni nabii!

Sasa unasema, "Loo, lakini huyo aliyefanya hivyo alikuwa mchawi."

80 Sawa, nitakwaambia Mmoja ambaye hakuwa mchawi. Yesu aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana, wakaenda kwenye Mlima wa Kugeuzwa wakati mmoja, naye alikuwa amesimama juu ya huo mlima. Na, Yesu, Mungu alikuwa akimweka Mwanawe mahali Pake; kama ninavyojaribu huu … tuliokuwa nao juzi usiku, kumweka mwana mahali pake. Na wakati walipofanya hivyo, waliangalia kila mahali na kuona ya kwamba pale walisimama Musa na Eliya. Walikuwa wakizungumza, wakishirikiana. Si bendera ndogo nyeupe zikipepea kila mahali, ama mawingu madogo meupe, ndiyo namaanisha, yakielea kila mahali. Lakini wao walikuwa ni watu, wakizungumza. Musa alikuwa amezikwa katika kaburi ambalo halikujulikana kwa miaka mia nane. Naye Eliya alikwishakwenda Nyumbani katika gari, miaka mia tano. Na hawa hapa wote wawili, wangali hai kama walivyopata kuwa hai, wakiwa wamesimama pale wakizungumza Naye kabla Yeye hajaenda Kalvari. Haleluya! "Kutiwa muhuri hata siku ya ukombozi wetu!"

81 Nitaharakisha, kisha tutafunga kwa sababu tmuda umeenda, nasi tutawaombea wagonjwa, kama dakika zingine tano. Aya ya 14, soma, hebu nisome aya ya 13, nipate, kuweka msingi.

*Nanyi katika huyo … mmekwisha kumwamini baada ya kusikia Neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; …*

Sasa kumbukeni, wana wokovu gani? Hawa walikuwa—hawa walikuwa Wakristo wa Efeso. Wao, sasa angalia, je! Mliona Wakorintho? Daima ilimbidi kuwaambia, "Nilipokuja kati yenu, mmoja ana lugha, mmoja ana lugha, mmoja ana zaburi, mmoja ana unabii, mmoja ana …" Unaona, yeye asingeweza kuwafundisha lolote, kwa sababu daima walikuwa wakitamani *hiki*, *kile* au *kinginecho*. Watu hawa walikuwa na jambo lile lile, bali walikuwa wameliweka katika utaratibu. Yeye kamwe hakuwafundisha Wakorintho kitu kama hiki, hakuweza, kanisa halikuwa kaika utaratibu ili kulifundisha. Sasa, yeye aliweza kuwafundisha watu hawa jambo halisi.

> … ambalo, *wokovu wenu; tena mmekwisha... kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu,*
>
> *Ndiye aliye arabuni* … (loo, hebu nisilipte hilo) … *arabuni ya urithi wetu ili kuleta … ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake. Whiu!*

82 Roho Mtakatifu ni nini? Sasa, basi nitasoma yaliyobakia upesi sana kama mtanivumilia kiasi hicho cha muda. Tulikuwa wapi usiku wa juzijuzi, Ndugu Mike? Pale ambapo wote walikuwa na furaha, loo, kila kitu kilikuwa ni amani, huo ulikuwa ni upendo mkamilifu. Sasa, kila mara unapokuja upande *huu* unashuka chini kidogo, unashuka. Kila wakati unapopiga hatua, unakaribia kwa inchi kadha. Inapofikia duniani, una kivuli cha kivuli cha kivuli cha vivuli. Sasa, hicho ndicho kiasi ulicho nacho ndani yako cha Roho Mtakatifu. Huo ni upendo. Lakini, loo, unaona kiu jambo fulani.

Ee, si watu kama wazee, wazee sana … Jinsi gani ningelipenda kurudi nyuma na kuwa na umri wa miaka kumi na tano tena, ishirini! Loo, ningetoa chochote kile. Ingenifaa nini? Huenda nikawa na umri wa miaka kumi na mitano na bado nife usiku wa leo. Haijulikani. Vipi kama ungekuwa na umri wa miaka kumi na mitano usiku wa leo, unajuaje kama mama angekuwa hai, unapofika nyumbani, ama la? Unajuaje utafika nyumbani? Unajuaje utakuwa hai kesho kama una umri wa miaka kumi na miwili, na afya kamilifu? Huenda ukauawa katika ajali, uanguke na kufa, jambo lolote linaweza kukutokea. Hakuna uhakika, unaona. Hakuna kitu kilicho na hakika hapa. Bali unatamani jambo hilo. Ni kitu gani? Ni Hicho kilicho kule Juu kikikufanya utamani jambo hilo.

83 Sasa, unaingia katika Hili, ndipo una Uzima wa Milele. Sasa inakuwaje? Ni "arabuni."

Arabuni ya fedha kwa chochote ni nini? Kama nikija kwakou kununua gari, niseme, "Gari hilo linauzwa bei gani?"

Unasema, "Gari hili, Ndugu Branham, linakugharimu dola elfu tatu."

"Malipo ya kwanza nikiasi gaini?"

"Vema, nitakuachia uchukue dola mia tano."

"Vema, hizi hapa dola mia tano. Nita—nitaleta zilizobakia wakati mwingine, kwa haraka niwezavyo. Wewe kaa na hilo gari." Nakupa dola mia tano, hiyo ndiyo arabuni. Hiyo ni kweli?

Sasa, shika hizo, ni "arabuni," ni "malipo ya kwanza."

> … baada ya *kutiwa muhuri kwa … Roho wa ahadi, … Roho wa ahadi, …* baada ya *kutiwa muhuri …*
>
> *Ndiye aliye …*

Nini, Muhuri wa ahadi ni nini, Roho wa ahadi aliye Mtakatifu?

> *Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta … ukombozi wa milki yake, …*

84 Ni kitu gani? Ni malipo ya kwanza. Na, ndugu, loo, loo, loo, loo, loo, loo, enyi wahubiri! Kama haya ndiyo malipo ya kwanza, itakuwaje wakati sisi sote tutakapofika kule! Itakuwaje? Kama haya ndiyo … Kama haya tunayofurahia sasa, na kuwa na furaha sana hata … Nimewaona watu wenye umri wa miaka tisini wakija tu …

Nimemwona mhubiri mmoja mzee aliyeinuka usiku mmoja. Akatoka, akasema … Namna *hii*, akija jukwaani. Nami nikasema, "Ati yule mzee aende kuhubiri?"

Akasema, "Vema, Bwana abarikiwe." Jamaa mzee mweusi, amevaa koti kubwa na refu la mhubiri lililochakaa.

Nikasema, "Kwa nini hakuwaachia baadhi ya hao wahubiri vijana wahubiri? Huyo mzee, anawezaje kuhubiri?"

Akasema, "Vema," akasema, "ndugu," akasema, "leo nimekuwa nikiwasikia ndugu wakihubiri mchana kutwa," akasema, "kuhusu yale Yesu aliyofanya duniani. Nitasimulia yale aliyofanya Mbinguni." Yeye

akasema, "Nitachukua somo langu usiku wa leo kutoka Ayubu 7:27," kasema, "ambapo ilikuwa ni huko nyuma kabisa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu," kasema, "wakati Yeye aliposema kwamba nyota za asubuhi ziliimba pamoja na wana wa Mungu. wakapiga kelele kwa furaha." Akaanza namna hiyo. Kasema, "Mnajua jambo hili, kuna kitu kilichokuwa kinaendelea huko nyuma." Akasema, "Mnajua …" Naye akaanza kuleta yale yaliyotukia Mbinguni. Akayaleta kwa njia ya upinde wa mvua uliolala sawa na nchi katika kule Kuja kwa pili. Yapata wakati huo, Roho Mtakatifu akamgusa. Sasa, iliwabidi kumwongoza jamaa huyo mzee njia, alikuwa na yapata umri wa miaka tisini na mitano. Yeye yuko *hivi* tu, ameinama mwili wote, na mzingo mdogo tu wa nywele, unajua, namna *hii*. Akatoka kwenda kukle na akaanza kuhubiri, kasema, "Masalale! Haleluya! Utukufu!" Akaanza kurukaruka namna hiyo. Kasema, "Loo, hakuna nafasi ya kutosha hapa kwa mimi kuhubiri." Ndipo akatimua mbio, sakafunu namna hiyo, kwa bidii awezavyo. Na hiyo ni arabuni tu. Loo!

85 Roho Mtakatifu hufanya nini? Loo, hapa pana mahali pazuri, hebu nisome aya ya kwanza ya sura inayofuata. Niisome? Ni sawa? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!" — Mh.] Vema, aya ya 1 ya sura ya 2, upesi. Sikilizeni. "Ninyi mliokuwa … *Ninyi …*"

> *Nanyi amewahuisha, mliokuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;*

"Ninyi ametuhuisha." Maana ya *kuhuishwa* ni nini? "Kufanywa hai." Karibu tu kwisha, bali Yeye amwahuisha tu kwa fedha za arabuni. Itakuwaje wakati u—wakati utakapopata faida yote ya gawio? Loo! Si ajabu Paulo, alipotwaliwa hata kwenye mbingu ya tatu, alisema, "Mambo ambayo jicho halikuyaona; sikio halikuyasikia; wala hayakuingia katika, hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia (amewawekea akiba) wampendao." Itakuwaje! Nena kuhusu furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu! Whiu! Uhm! Ninyi mliokuwa mmekufa katika dhambi na makosa Yeye ametuhuisha pamoja kwa kivuli cha kivuli wa vivuli. Itakuwaje utakapofikia kwenye kivuli cha vivuli kisha uingie katika kivuli, kivuli kisha uingie katika kijito, kijito kisha uingie mtoni, mtoni uingie baharini?

86 Na ni nini unapokuwa huko mbali sana katika ukombozi, umevikwa mwili mpya kabisa, umerereja na kuwa mwanamume kijana kabisa tena, ama msichana, hutakufa tena kamwe? Nawe unaangalia chini duniani, na kuwazia, "Ningeweza kufurahia zabibu na maji mazuri ya baridi, lakini, unajua, sivihitaji hivyo hapa. Bali siku moja Yesu yuaja, na mwili huu wa kimalaika, mwili huu wa kiungu ninamoishi ndani …" Hauitapitia kwenye tumbo la uzazi la mwanamke tena, hautapitia tena kwenye tamaa ya kujuana kimwili; lakini kwa sababu Yeye alizaliwa pasipo tamaa ya kujuana kimwili, nitafufuliwa bila hiyo, Naye atanena siku moja nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa, na huo mwili ambao wakati mmoja niliishi humo utafufuliwa uwe mwili uliotukuzwa, nami nitatembea na nitazungumza, nami nitaishi na kufurahia (haleluya), nitaishi katika nyakati za Milele zitakazokuja, katika Yesu Kristo Bwana wetu. Whiu! Haya basi, ndugu, hiyo ndiyo Injili!

87 "Kwa sababu hiyo mimi nami," Paulo akisimulia tu sasa jinsi alivyo. Nitasoma haya yaliyosalia kisha tuwaombee wagonjwa. "Hata katika ile milki, arabuni hii itadumu hadi kwenye ile milki, kwa sifa za utukufu Wake."

> *Kwa sababu hiyo mimi nami, tangu nilipopata habari za imani yenu* (Nilisikia kwamba mliamini jambo hili, nilisikia kwamba kweli mliamini katika kuchaguliwa tangu awali, Uzima wa Milele, na wokovu, na kadhalika) *katika Bwana Yesu, na pendo lenu kwa wote … watakatifu,*
>
> *Siachi kutoa shukrani zenu kwa ajili yenu; nikiwakumbuka katika sala zangu;*
>
> *Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo … kumjua yeye:* aendelee tu kujifunua Mwenyewe kwenu wakati wote, mkikua kutoka neema hadi neema, kutoka nguvu hata nguvu, utukufu hata utukufu. Si kurudi nyuma; na, bali kutoka utukufu hata utukufu, muendelee kusonga mbele. Nitaendelea kuwaombea.
>
> *Ma—macho ya mioyo yenu …*

88 Ala! Unajua, katika Biblia ilisema ulikuwa kipofu na hukujua. Lakini hapa Paulo alisema, "Nitaomba kwamba macho ya mioyo yenu …" Unaelewa kwa moyo wako. Hilo ndilo analozungumzia. Unaangalia kwa jicho lako, bali unaona kwa moyo wako. Unajua hivyo. Vema. "Kwamba Mungu wa Utukufu …" Hebu tuone, a-aya ya 18.

> *Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru; mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo, na utajiri wa … utukufu wa urithi wake katika watakatifu ulivyo;*
>
> *Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yenu,* (Whiw! Wanasema nguvu zimekwisha? Nguvu hata hazijafika bado) ... *tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake;* (Ninyi ambao mmeamini kutenda kazi kwa nguvu Zake kuu, naomba tu kwamba Mungu atazimwaga tu nguvu Zake juu yenu. Mnaona?)

*Aliotenda katika Kristo, alipomfufua katika-katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika … maeneo ya kimbinguni,*

*Juu sana … falme, … mamlaka, … nguvu, … usulutani, na* kwamba *kila jina litajwalo, …*

Loo, loo, loo! Kwa- … La, afadhali niache hayo. Hakika tungechukua usiku uliosalia juu ya jambo hilo.

*… kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao;*

89 Ni nini kila—ni nini kila jina? Kila jina la kila mtu litakuwa na Jina la nini? [Kusanyiko linasema, "Yesu." — Mh.] Mbingu yote inaitwa Yesu. Kanisa lote linaitwa Yesu. Kila kitu kinaitwa Yesu, kwa kuwa ndilo Jina pekee ambalo Mungu amewahi kuwa nalo. Yeye anaitwa Yehova; Yehova-yire, Dhabihu iliyotolewa na Bwana; Yehova-rafa, Bwana akuponyaye; Yehova, beramu ya Bwana, Wamanase; na Yehova, Yehova mbalimbali. Yeye anaitwa Nyota ya Asubuhi. Anaitwa Baba, anaitwa Mwana, anaitwa Roho Mtakatifu. Yeye anaitwa Alfa, anaitwa Omega. Yeye anaitwa Mwanzo, anaitwa Mwisho. Yeye anaitwa Tawi. Loo, Yeye anaitwa … Yeye anaitwa tu kila aina za sifa, bali alikuwa na Jina moja.

Hilo ndilo Mathayo alilokuwa akizungumzia, wakati aliposema, "Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina," si katika majina, "katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Baba si jina, Mwana si jina, Roho Mtakatifu si jina. Ni cheo cha Jina. Ni Jina lenye sifa tatu ambazo ni za Mungu mmoja. Jina Lake lilikuwa nani? Yule Malaika alisema, "Utamwita Jina Lake …" [Kusanyiko linasema, "Yesu." — Mh.] "kwa maana atawaokoa watu Wake na dhambi zao." Hiyo ndiyo sababu wote walibatiza hivyo katika Biblia. Hivyo ndivyo Mtakatifu Agostino alivyombatiza Mfalme wa Uingereza, yapata—yapata miaka mia moja na hamsini, miaka mia mbili baada ya kifo cha Kristo, katika Jina la Yesu Kristo. Vema.

*Juu sana … falme, … mamlaka, … nguvu, … usultani, na kila jina litatajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia;*

*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa,*

*Ambalo ndilo mwili wake, …*

90 Sasa, kama mwili wangu una mamlaka juu ya vitu vyote, basi vile ulivyo mwili wangu ndivyo nilivyo mimi. Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo nilivyo, hivyo ndivyo mnavyonijua mimi. Hiyo ni kweli? Vema, basi, yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamwaga ndani ya Yesu, kwa kuwa Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Hiyo ni kweli? Na yote aliyokuwa Yesu, aliyamwaga Kanisani, "Mambo haya niyafanyayo, ninyi nanyi mtayafanya mambo yote pia. Hata maku zaidi kuliko haya mtayafanya, kwa maana naenda kwa Baba."

*Ndio mwili wake, utimilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*

91 Loo, jinsi ninavyopenda jambo hilo! Jinsi ninavyopenda jambo hilo! Nilikuwa nikisoma hivi majuzi kitabu kilichoandikwa juu ya ziarai niliyofanya ya kwenda ku-kuhudumu Afrika. Kamwe sijawahi kukisoma hapo kabla. Ni wangapi waliopata kukisoma hicho kitabu, *Nabii Azuru Afrika*? Mle ndani nilikuwa nikimwangalia mvulana mdogo wa Kihindi. Ni wangapi walioiona picha hiyo?

Nilimsikia mwinjilisti fulani, aliyekuwa akiwaombea wagonjwa kwa yapata miaka kumi na mitano au zaidi, alisema, "Sijapata kuona muujiza ukitendeka maishani mwangu." Akasema, "Nimewaona watu waliosema walikuwa wanaumwa na kichwa, wameta afya. Nimeona watu wakisema walikuwa wanaumwa na tumbo, wakapata afya, na kadhalika. Lakini muujiza, kitu kilichoumbwa na kufanya kitu …"

Nikafikiri laiti mvulana huyo angalikuwa amesimama pale apate kuona jambo hilo. Mguu wa mvulana huyo wa Kihindi ulikuwa karibia mnene "hivi*, mmoja. Huo mwingine ulikuwa ni mguu wa kawaida kama mguu wa mwanadamu. Na, kama mkiangalia, gango lake, kulikuwa na kiatu chake cha kama urefu wa inchi kumi na nne ama inchi kumi na tano kama hivi. Alikuwa na bamba la chuma kwenye upande wake wa chini. Kiatu chake kiliwekwa kwenye nguzo mbili zilizosimama. Alitembea mpaka mahali nilipokuwa nimesimama, wakamleta pale. Alikuwa na mikongojo miwili. Yeye akachukua kiatu hiki kikubwa cha chuma na kukanyaga nacho chini kwa kishindo namna hiyo. Nikauangalia mguu wake, ulikuwa karibu mnene *hivi*.

92 Sasa, hao watu ni Waislamu, Waislamu. Mnakumbuka Jumapili iliyopita nilipowasomea yale magazeti yaliyolazimika kuandika? Ninayo papa hapa mimi mwenyewe, kutoka Afrika, niliyotumiwa na mmishenari wetu aliyerudi, Ndugu Stricker. Humo kuna makala jinsi Billy Graham alivyoepa jambo hilo. Kweli kabisa. Wao walimwacha huyo Mwislamu akimsukuma moja kwa moja hata baharini. Kuna nini? Wamishenari wanaondoka uwanjani. Kuna faida gani ya kukaa zaidi, wameshindwa tu.

Nampenda Billy Graham, na nafikiri yeye ni mtu mzuri sana wa Mungu. Lakini kile ambacho Billy Graham alipaswa kumshambulia nacho, aseme, "Ngoja kidogo …" kama baadhi ya hawa Wabatisti wa kidesturi wangemruhusu afanye jambo hilo, naamini angefanya hivyo. Ninaamini Billy Graham ni mtu wa

Mungu. Lakini kama angalisema, "Ngoja kidogo! Mimi ni mhudumu wa Injili. Mnaamini katika Agano la Kale, nanyi mlisema ya kwamba Yesu hakuwa kitu ila mwanadamu. Nawasai mje tujadiliane." Mimi siamini katika kujibu sai za ibilisi, la bwana, bali mimi ningelimsai pia, na kusema, "Hebu wewe na mimi tukutane. Mimi ni Daktari wa Theolojia, "Billy Graham ni Daktari wa Theolojia. "Hebu nikusai juu ya jambo hili, na hebu nikuthibitishie ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo. Sasa, kwa habari za uponyaji wa Kiungu, mimi sina karama hizo, bali tuna baadhi ya ndugu walio nazo. Sasa, kama unataka kuwaleta hao watu huko nje, hebu nimpigie simu mmoja wao, Oral Roberts ama mtu fulani, mtu fulani aliye na huduma kuu ambayo kweli angefika kule." Waje kule, kisha waone kitakachotukia, aseme, "Ukristo si vile mnavyofikiria kuwa uko."

93 Sasa kila mtu anajisikia ametahayarishwa kwa sababu yeye aliondoka tu akamwacha. Bila shaka, sasa, siamini ibilisi akikupa changamoto. Mimi nimemtemea mate usoni pia namna hiyo, nikaondoka nikamwacha. Hiyo ni kweli. Lakini inapofikia mahali ambapo … Billy angali—angemfanya Mwislamu huyo ajisikie kama gugu dogo namna *hiyo*. Yeye angaliweza kuichukua hiyo Biblia na kuchukua Isaya 9:6, na kusema, "Yeye alikuwa akinena habari za nani, 'Maana kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume'? Mtu huyu alikuwa ni nani? Ni nani huyu aliyekuwa akizungumzia habari Zake? Nabii huyu alikuwa nani? Huyu Masihi aliyekuwa aje alikuwa ni nani? Nionyeshe mahali alipojitdhihirisha katika Mohammed. 'Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.' Nionyeshe hayo katika Mohammed. Yeye aliliaje, 'Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Wameichoma mikono Yangu na miguu Yangu, 'na kadhalika? Nionyeshe kwa neno lenu wenyewe, agano lenu wenyewe." Mbona, yeye angemshinda huyo Mwislamu vibaya sana hata asingejua mahali alikokuwa. Hiyo ni kweli.

94 Lakini wakati gazeti lilipolazimika kugeuka, hilo ndilo lililohuzunisha, lililoufanya moyo wangu uruke. Wakati iliposema mle, "Ingawa ilimlazimu Billy kuepa na akaepa, Waislamu wanawezaje kusema kwamba ilikuwa ni kosa," kasema, "na huku Kasisi William Branham kule Durban, Afrika Kusini, alifanya muujiza usioweza kubishaniwa kabisa mmoja baada ya mwingine, nguvu za Kiungu, wakati Waislamu elfu kumi walipoanguka kifudifudi kwa wakati mmoja na kuyatoa maisha yao kwa Yesu Kristo." Kabisa. Wanajua habari zake. Hao wa asilia wanajua habari zake. Usiniambie.

Wakati mmoja kulikuwa na mmoja aliyemjia Yesu, akasema, "Rabi!" Mnajua alikuwa Mfarisayo. Kasema, "Tunajua Wewe ni Mwalimu aliyetoka kwa Mungu. Tunajua hivyo. Tunajua hivyo, maana hakuna mtu angeweza kufanya mambo unayoyafanya Wewe isipokuwa Mungu awe pamoja naye. Tunafahamu. Tunajua hivyo. Lakini hatuwezi kabisa kukiri jambo hilo, unaona, maana tukifanya hivyo, vema, tutafukuzwa kanisani mwetu. Mnaona, tutapoteza heshima yetu." Na kwa hiyo Yesu akasema, akaanza kumwambia hana budi kuzaliwa mara ya pili.

95 Juu ya huyo mvulana wa Kiislamu, wakati alipokuwa amesimama pale, ile pale picha yake. Kamera haiwezi kupiga uongo picha. Huyo pale amesimama pale, huku mguu mmoja ukiwa mfupi kadiri hiyo (yapata inchi kumi na nne) kuliko huo mwingine, akiwa amesimama kwenye kiatu hicho cha chuma. Nikamwambia, nikasema, "Unazungumza Kiingereza?"

"La, bwana." Asingeweza kuzungumza Kiingereza. Mkalimani akasema, "Yeye hazungumzi Kiingereza."

"Umekuwa hivyo kwa muda gani?" Yule mkalimani akamwuliza.

"Tangu kuzaliwa."

"Je! Unaweza kusogeza huo mguu hata kidogo?"

"La, bwana."

"Je! Unamwamini Yesu Kristo?"

Kasema, "Mimi ni Mwislamu."

Nikasema, "Je! Utamkubali Yesu Kristo kama atakuponya?"

"Nitamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu iwapo ataniponya."

"Kama atauponya huo, huo mguu uwe kama ule mwingine, utamkubali?"

"Nitamkubali."

96 "Vema, Mungu, utafanyeje?" Hili ndilo jambo lifuatalo; maswali yote yamejibiwa. Ndugu Mike, huko ndiko kuhisi. Nangojea tu kidogo kuona Yeye atakalosema. Nikaangalia kule nikamwona mvulana huyo akienda, akitembea, kama kando ya kuta namna hiyo. Nikasema, "Ni wangapi wenu ninyi Waislamu mtakubali jambo hilo? Huyu hapa mvulana wa Kiislamu, mwangalieni, msimamisheni pale." Nikasema, "Ninyi madaktari, mnataka kumchunguza? Huyo amesimama hapo." Loo, unajua ulipo wakati huo. Unaona, unajua mahali unaposimama. Hakuna mtu … Huyo hapo.

Nikasema, "Pita upande huu, mwanangu." Nao wakamwongoza, huyu hapa anakuja. ("Ta-lump, ta-lump.") Nikasema, "Unaonekana mfupi kwa yapata inchi kumi na mbili, kumi na nne. Kama *hivyo*."

"Naam."

Nikasema, "Lakini Yesu Kristo Mwana wa Mungu anaweza kumponya. Je! Ninyi Waislamu mtaamini na kumpokea kama Mwokozi binafsi?"

Kuna maelfu ya hiyo mikono myeusi iliyoinuliwa juu namna hvyo. "Vema, Bwana, sasa huu ndio wakati." Nikasema, "Baba wa Mbinguni, kama uliwahi kujibu, nijibu sasa, hili ni kwa ajili ya Utukufu Wako, hili ni kwa ajili Yako. Naomba Wewe mponye mvulana huyu." Nilimwombea tu namna hiyo.

Nikasema, "Vua kiatu chako." Aliniangalia isivyo kawaida kabisa, yule mkalimani. Nikasema, "Vua kiatu chako." Akakifungua. Kwa sababu tayari nimeona ono hilo, yale yatakayotukia. Yeye akavua kitu hicho. Wakati alipokirudisha na kutembea pale akinijia, huku miguu yote miwili ni ya kawaida kabisa, huku yote miwilii ikitembea kama mipya. Nikasema, "Unataka kutembea huku na huko?"

Alianza kulia namna hiyo, akienda huku na huko, hakujua la kufanya. Akitembea namna hiyo, akasema, "Ee Allah! Allah!"

Nikasema, "Yesu! Yesu!"

Loo, loo, loo! "Ee Yesu! Yesu," basi. "Yesu! Yesu," namna hiyo.

Nikasema, "Kuna maswali yo yote, maswali yo yote?"

97 Julius Stadsklev, ni wangapi wanaomjua? Ndugu Stadsklev anayekuja hapa kanisani; ndiyo—ndiyo kwanza aende Ujerumani. Kasema, "Hebu kidogo, Ndugu Branham, hebu kidogo." Tumlete mpiga picha upesi sana. "Naweza kumpiga picha?"

Nikasema, "Utakavyo."

"*Njoo hapa*, simama kiatu chako *hapa*." Akasimama namna hiyo, akapiga picha ya huyo mvulana pale, huku miguu yote miwili ikiwa mizima na imenyoka iwezavyo kuwa. Hicho hapo kiatu chake cha zamani na gango, namna *hiyo*, namna *hiyo*.

Nikasema, "Ni wangapi wenu ninyi Waislamu sasa wanamkataa Mohammed kama nabii, na kumwamini Yesu kama Mwana wa Mungu, na kumkubali kama Mwokozi wenu binafsi?" Mikono elfu kumi ikainuliwa hewani. Haleluya! Hawataki ninii …

98 Wao wanajaribu kulificha, kwa sababu sisi ni "watakatifu wanaojifingirisha," ndivyo wanavyotuita, unaona. Yote ni mamoja, Mungu anatenda kazi. Yeye analiweka Kanisa Lake mahali pake. Yeye anafanya mambo mengi mno, mengi mno kuliko yote ambayo tungeweza kufanya ama kuwazia. Yeye yungali ni Mungu tu usiku huu kama vile Yeye alivyowahi kuwa.

Kwa hiyo, enyi marafiki wadogo, hebu niwaambieni jambo fulani sasa hivi. Enyi watu wangu wapenzi na wa thamani, ninyi mlio hapa katika nchi hii, na wengine katika nchi zilizo na kanda ambao mtakuwa nkatika chi za ng'ambo na popote mlipo, msiogope. Kila kitu ni sawa. Baba Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alijua kila kitu ambacho kingetukia. Kila kitu kinaftendaka moja kwa moja. Mnampenda? Weka moyo wako sawa.

99 Na, kumbukeni, wakati pumzi hii inapopita kutoka kwenye maisha haya, kwenu ninyi wazee ama kwenu ninyi vijana, na ninyi akina mama, mtakapowaona watoto wenu wachanga, mtoto huyo mchanga wa kike aliyekufa wakati hakuwa na umri wa siku nane ama siku tano, yeye atakuwa msichana mrembo utakapomwona. Huyo Babu mzee aliyeinama kabisa, ilikuwa vigumu kwake kuona mahali alikokuwa akienda; utakapomwona, bibi kizee, atakuwa kijana mzuri mwenye sura nzuri, kijana tu mwenye umri mdogo kama wa miaka ishirini, akiwa tu katika fahari ya ujana. Naye atakuwa jinsi hiyo milele. Unaweza kugusa mkono wake, unaweza kupeana mikono naye. Utamkumbatia, lakini yeye hatakuwa "mume," atakuwa "ndugu." Loo, jamani! Yeye atakuwa wa hali ya juu sana kuliko vile "mume." Unafikiri ulimpenda? Hakika ulimpenda. Lakini huo ulikuwa wa *phileo*; subiri mpaka uupate ule wa *agapao*. Ngojeni mpaka huo upendo halisi wa Kiungu ushike, ndipo uone ni nini. Huu hapa ni kama jalala la kale linalofuka moshi, hauna faida, haufai kitu. Jambo pekee ninawashauri kufanya sasa, ni hili, ra—ra-razangu zangu …

100 Baadaye kidogo nita- … Mngetaka nizichukue hizo sura zingine mbili wakati mwingine? Bwana … Ina—inanibidi kupumzika kidogo tu kabla ya Chautauqua. Sasa, siwezi kuhubiri mambo haya katika mikutano hiyo. Kuna ninii nyingi sana ya- … imani nyingi sana mbalimbali. Mnaona? Hili ni kanisa pekee. Unaona? Siwezi … Nina haki ya kuhubiri humu ndani cho chote ninachotaka. Hii ni maskani yangu, mnaona, nami nawaambieni. Sasa, naamini watu hao wameokolewa. Naam, bwana, kweli naamini. Lakini, loo, ni vizuri vipi kutembea unapojua mahali unapotembea. Ni vizuri vipi, kujua, kujua tu unalofanya, unaona, badala ya kuyumbayumba, ukijikwaa. Hebu na tusimame tu Nuruni, na tutembee katika Nuru na kujua

unakoelekea. Hiyo ni kweli. Bwana awe pamoja nanyi.

101 Na kama kila mmoja wenu humu sasa hajawekwa mahali pake! Huenda usiwe kitu ila mke wa nyumbani. Vema, unasema, "Ndugu Branham, sijafanya kitu maishani mwangu. Mimi si mhubiri." Vema, huenda Mungu alikuleta hapa upate kulea familia ya watoto, kutoka kwenye familia hiyo ya watoto huenda ikaja familia nyingine ya watoto ambamo ataktoka mhubiri ambaye atawapeleka watu milioni moja kwa Kristo. Ilibidi uwepo hapa. Uko hapa kwa kusudi fulani. Je! Ulijua jambo hilo?

Vema, unasema, "Yote niliyowahi kufanya, ilikuwa, kulima madonge haya ya kale. Nami ningetoka, mapema jioni, sikujua jinsi ya kuwapa watoto wangu riziki. Niliwaangalia maskini jamaa hawa wadogo wasio na viatu. Nimeketi na kulia. Nina gari la zamani, nami na Maw tulienda kanisani." Usijali, ndugu. Endeleeni tu kumpenda, Yeye ana kusudi na wewe. Wewe kaa tu jinsi ulivyo, endelea tu mbele moja kwa moja. Unaona? Huenda usihubiri hata somo moja, bali huenda ukawa baba wa mzaa babu na mtu atakayehubiri.

102 Je! Ulijua ya kwamba Mungu alimhesabia (hebu tuone sasa, jina lake lilikuwa nani?) Lawi, kulipa fungu la kumi wakati alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu, wakati Melkizedeki alipokutana naye. Ni wangapi wanaojua hilo? Na hebu tuone. Ibrahimu akamzaa Isaka, Isaka akamzaa Yakobo, Yakobo akamzaa Lawi; ambaye alikuwa baba, babu, baba mzaa babu; alipokuwa viunoni, katika mbegu ya baba mzaa babu yake, Biblia ilimhesabia amelipa fungu la kumi kwa Melkizedeki. Jamani, jamani, jamani, jamani! Ndugu! Loo! Mimi …

103 Kuna maskini—kuna maskini Mwingereza mmoja aliyeongoka usiku mmoja huko Uingereza, akasema, "Nina furaha sana! Nina furaha sana!"

Naam, nina furaha sana kujua ya kwamba hiyo ni kweli! Na siku moja yenye utukufu, sijui siku hiyo itakuwa lini, lakini kama hilo lilikuwa ni ono, sisemi nilikuwa hapa. Kumbuka, daima kumbukeni jambo hili, na wenye kanda wafanye vivyo hivyo. Kwamba nilikuwa katika ono, ama kuchukuliwa katika Roho, mimi sijui. Lakini ilikuwa halisi tu kama ninavyomshika Ndugu yangu Neville namna *hiyo*, ni halisi tu jinsi hiyo. Nami ningeweza kuwatazama na kuzungumza na hao watu. Na pale alisimama mke wangu wa kwanza, yeye hakupaza sauti "mume wangu," alisema, "ndugu yangu mpendwa."

Hapo alisimama msichana niliyezoea kuandamana naye miaka kadha iliyopita.

104 Labda baadhi ya watu wake wanameketi hapa, Alice Lewis kutokea Utica, msichana mzuri sana, Mkristo mwaminifu. Alichelewa kidogo kuolewa maishani, naye akapata mtoto wake wa kwanza na akafa katika kuzaa. Alice Lewis, nilienda katika shirika la kuzika wafu kumwona. Nilikuwa nimerudi tu nyumbani, nikasikia amekufa. Nikaenda kule, hakukuwa na mtu mle chumbani, nikasema, "Je! Kuna mwanamke hapa, Bibi …" Jina lake lilikuwa Emmerke. Naye aliolewa na mvulana mzuri Mkristo, naye alikuwa msichana mzuri Mkristo. Nimekuwa pamoja na msichana huyo kila mahali, mahali pa kila namna na kila kitu. Nasi ni watoto tu, umri wa miaka kumi na nane, kumi na tisa, kila mahali, Mkristo mzuri, kamwe sikujua kitu juu yake ila Ukristo halisi. Nami nilikuwa mwenye dhambi. Lakini ningeambatana naye. Nikaingia kwenye… Naye mumewe alikuwa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mwanamume halisi. Nami sikujua; nilijua alikuwa amekufa, nilikuwa nimeona hilo kwenye gazeti. Nami nikashuka nikaenda kule nao wakaniambia. Nilishuka nikaenda kule kwa Coots na nikasema, "Je! Mna Bibi Emmerke?"

Akasema, "Billy, yuko moja kwa moja katika chumba kile."

Nikaingia mle na kusimama pale karibu na jeneza. Nikawaza, "Alice, nimekuwa katika magereza ya chini ya ngome zenye giza. Mimi na wewe tumetembea pamoja barabarani na kushuka tukaenda karibu na mto, wakati walipokuwa na ile mitumbwi ya zamani ya fahari, tungeketi pale na kusikiliza kinanda cha filimbi kikicheza. Huko na huko kwenye vichochoro vya njia, jinsi ulivyokuwa bibiye wa heshima! Jinsi ninavyomshukuru Mungu kwa ajili ya maisha yako. Pumzika, dada yangu mpenzi, pumzika katika amani ya Mungu."

105 Na usiku wa juzijuzi katika lile ono, huyo hapo anakuja akinikimbilia. Akasema, "Ndugu yangu aliyebarikiwa," kisha akanikumbatia kwa mikono yake. Loo, loo, ndugu na dada, jambo hilo lilinibadilisha. Siwezi kamwe kuwa vile vile tena. Ni halisi sana! Ni ninii tu—ni halisi tu kama ninavyowaangalia ninyi, halisi tu namna hiyo. Kwa hiyo, hakuna hofu. Huenda nikafa kabla ya usiku huu kwisha.

Nataka kumlea mvulana wangu mdogo kule nyuma, Joseph. Nataka kumwona mimbarani, wakati ambapo naweza kuichukua Biblia hii … nitakapofika mahali ninapoweza kumwona Joseph mimbarani akihubiri kama—kama kijana mwanamume aliyejazwa na Roho Mtakatifu, amepakwa upako na Roho wa Mungu juu yake. . Nami naamini atakuwa nabii. Siku ambayo ni—nilipo—nilipomwona miaka sita kabla hajazaliwa, mnakumbuka nikiwaambia alikuwa anakuja. Kumbukeni nilivyomwita, pale pale karibu na madhabahu, bila kujua nilichokuwa nikisema, huku nikiwaweka watoto wachanga wakfu, nilisema, "Joseph, wewe ni nabii."

106 Na hivi majuzi akiwa amesimama kule nje uani, alinijia, na akasema, "Baba, je! Yesu ana mkono kama

wako?”

Nami nikasema, “Vema, naam, mwanangu. Kwa nini?”

Akasema, “Nilikuwa nimeketi kwenye baiskeli yangu, nikimgojea Sara” (huyo ni dada yake mdogo) “arudi nyumbani kutoka shuleni.” Ameketi huko nje. Nisingemruhusu aende kule nje barabarani, alikuwa ameketi nyuma namna hii. Kisha akasema, “Nikaangalia juu, na,” kasema, “nilipoangalia, palitokea mkono kama wako, wa vazi jeupe la mkono mrefu ukinishikilia.” Kisha akasema, “Ulirudi juu.” Kasema, “Je, Huo uliorudi juu ni mkono wa Yesu?” Nikamwangalia mama yake, mama yake akanitazama. Tulishuka kwenda kwa Bi Woods. Popote alipo, ameeti hapa. Tukamhojihoji, kwa kila hali, na kwa kila njia tuliyoweza. Lilikuwa ono. Yeye aliliona. Ninapoweza kuona huo wakati ambapo mtoto Joseph anasimama … Natumaini nitaishi hadi nimwone ameoa, kama Yesu akikawia.

107 Nami ni mzee, sharafa zenye mvi zikiwa zinakining'inia humu shingoni mwangu hapa. Nimetuma … nataka kutuma nafsi milioni mbili ama tatu zaidi kwa Kristo kama naweza. Nimeazimia kuhubiri Injili kwenye kila pembe ya dunia. Ndio, bwana. Kwa hiyo, nisaidie, Ee Mungu, nitafanya hivyo. Kwa hiyo, laiti ningaliweza kuona wakati huo ukiwadia, Ndugu Mike.

Naweza kuangalia wakati ule Mama, Meda, ndivyo nimwitavyo, kipenzi changu, unaona, yeye … sisi tunazeeka, naona nywele zake zikipata mvi, kisha naona sisi tukiondoka, tukififia.

Rebeka, ninashukuru sana kwa ajili ya Rebeka. Mwalimu wake wa muziki aliniambia hivi majuzi usiku, akasema, “Jamani, akiendelea na jitihada hizo, Ndugu Branham,” anasema, “ni vigumu kujua atakalofanya.” Unaona, akiendelea katika muziki. Namtaka yeye, nami nataka … Namtaka Sara ashike kinanda, Becky naye ashike piano, namtaka Joseph mimbarani.

108 Wakati ninapoweza kuona jambo hilo likitokia, na mimi pamoja na Mama yake tunaweza kuingia huku tunakongoja, mimi na mkongojo wangu wa kale, usiku fulani, nashuka naja barabarani, nami naweza kuangalia mle ndani na kumwona mwanangu amesimama mle huku amejazwa na Roho Mtakatifu, akihubiri Injili hii hii. Nataka kuchukua Kitabu hiki cha kale, na kusema, “Mwanangu, Hiki hapa, Ni chako. Wewe simama Nacho, usiwe na suluhu juu ya Neno moja. Wewe dumu moja kwa moja Nacho, mpenzi. Usi-, sijali, sijali ni nani anayekupinga, anayepinga, Mungu atakuwa upande wako. Wewe hubiri kila Neno jinsi tu lilivyoandikwa Mle ndani, naye Baba atakuvusha ule mto.” Ningetaka kusogea na kumchukua mikononi mwangu, mke wangu, na kuuvuka Yordani.

Hata wakati huo, Mungu, hebu nijalie nidumu uwanjani, mwaminifu! Nijalie! Sijali gharama yake ni nini, ama ni wangapi, nifanyacho, ama *hili*, *lile* au *lingine*. Nijalie nidumu mwaminifu na wa kweli kwa Neno la Mungu aliye hai, ili kwamba siku hiyo itakapowadia nami nivuke ng'ambo ya pili ndipo naweza kuangalia upande wa pili na kusema, “Haya basi. Loo, rafiki yangu wa thamani, ndugu yangu wa thamani, dada yangu wa thamani.”

109 Ewe mhubiri mchanga, ingia uwanjani, dumu kwenye hatamu. Enyi wahubiri wachanga wote na kadhalika, msiketi kitako hapa. Msiketi tu na kutofanya lolote. Ondokeni mwende kule mkaokoe nafsi. Fanya jambo fulani! Hima, shikeni njia mwende. Usikome, ewe mhubiri mchanga kule. Mungu na aubariki moyo wako.

Yeye ananikumbusha wakati nilipokuwa na umri kama huo, nadhani, na labda kijana zaidi kidogo kuliko yeye. Nilikuwa na umri wa miaka ishirini na kitu tu wakati nilipoweka jiwe lile la pembeni pale. Nakumbuka nilikuwa nikivaa koti la bluu na suruali nyeupe, nami nikasimama pale na kuliweka jiwe lile la pembeni yapata miaka thelathini na moja iliyopita. Mnaona nilkuwa na umri gani, nilikuwa mvulana tu. Nikasimama tu pale, nikiliweka lile jiwe la pembeni. Sijawa na suluhu juu ya Neno moja. Nimeliweka jinsi hasa lilivyokuwa nilipoliweka lile jiwe la pembeni. Ule pale ushuhuda wangu umewekwa pale, mahali nilpoiuandika kwenye ukurasa wa kwanza wa Biblia yangu, kisha nikaurarua na kuuweka kwenye lile jiwe la pembeni, na ungali uko pale. Na jalia uandindikwe kwenye kurasa za Neno la Mungu la Milele Mbinguni. Naomba nidumu mwaminifu hata mwisho.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda kidogo tu kwa maombi.

110 Katika kufunga usiku huu, tukifunga kwa haya, sura moja, jambo ambalo si halali. Mnapaswa kupata hiyo nyingine, na jinsi anavyosonga mbele na kuliweka kanisa mahali pake. Nitawaletea hilo wakati mwingine, Mungu akipenda. Inanibidi kupumzika kidogo sasa kabla sijaenda huko Chautauqua, kwenye mkutano mwingine mkubwa, kisha nivuke kutoka huko niende Oklahoma, kutoka hapo niende hadi Klamath Falls, kisha kutoka Klamath Falls na kuendelea hadi California, hadi kuingia Yakima, sitarudi mpaka Agosti ijayo tarehe 15.

Lakini angalieni, hebu niwaulizeni jambo fulani, kama jambo fulani lingewatokea au mimi kabla huo wakati haujaja, kama ningevuka kule mtoni kuingia ile Nchi, au kama ninyi mtavuka kule kabla ya wakati huo kuingia katika ile Nchi, je, unayo hakika usiku huu kwamba tutakutana kule katika ile sehemu? Kama unayo hakika, inua mkono wako juu, useme, “Najisikia hakikisho moyoni mwangu.” Mungu na aubariki

moyo wako. Mungu akubariki. Kama kuna mmoja hapa ambaye hajisikii hakikisho la kwamba wangekuwa kule, na angetaka kusema, "Nikumbuke, Ndugu Branham, ya kwamba nitakuwa na hakikisho hilo," inua mkono wako juu, "ninataka kuwa pale , pia." Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki.

Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe usiku wa leo kusanyiko hili, kila mkono, nijuavyo mimi, ulikuwa juu. Wote ila mtu mmoja, nafsi fulani ya thamani iliyoketi hapa nyuma, wamechoka tu kidogo kama wangeweza kuvuka kwenye ile nchi, ambako kuna upendo halisi wa Kiungu mioyoni mwao, katika moyo wa mwanamke huyo wa thamani, kwamba angekuja kwenye nchi hiyo kama alikuwa afe usiku huu: je, huo ungeivuta nafsi yake iliyochoka kuingia katika Nchi ya Ahadi ya Mungu?

Baba wa Mbinguni, kama nilivyosimama hapa kwenye mimbara hii na kuhubiri, na kutokwa jasho, na kulia, na kuomba, na kushawishi, hebu nikuombe mara nyingine tena, Bwana, hebu niombe kwa ajili ya dada yangu nyuma pale; Mungu, weka ndani ya moyo wake usiku wa leo: upendo huo wa Kiungu, huyo Roho Mtakatifu wa Mungu, ile amani ipitayo akili zote, kwamba angempokea Roho Wako, atiwe muhuri na Roho Mtakatifu mpaka siku ile. Nataka kumwona, Bwana, tutakapovuka lile daraja. Kama ni—kama ni ninii yangu—kama ni majaliwa yangu kuvuka, kama yale uliyonionyesha ni halisi, nami navuka kule, nataka kukutana naye pale, na kumwona akikimbia na kunishika mkono, na kusema, "Ndugu yangu wa thamani, ilikuwa usiku ule ambapo Kitu fulani kiliniambia niinue mkono wangu juu, ulipomaliza kuhubiri juu ya kitabu cha Efeso. Nikainua mkono wangu juu, na jambo fulani likanitokea baada ya jambo hilo. Ndio huyu mimi hapa. Mimi ni kijana sasa milele." Mungu na amjalie huyo wa thamani.

Hawa ambao wameinua mikono yao juu kwamba wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu yu juu yao, nao wamempokea Roho Mtakatifu, wametiwa muhuri kwa upendo huo wa Kiungu mioyoni mwao. Tunakushukuruje kwa ajili yao.

Tukitambua, Baba, ya kwamba kanda hizi zitaenda ulimwenguni. Vipasa sauti vingi vimesambazwa kwenye mimbara hii, ikimaanisha kwamba kanda zinatengenezwa, zikirudi kule nyuma, ile Sauti itakuwa ikienda katika nchi mbalimbali kote ulimwenguni, kote ulimwenguni, mataifa ishirini ama thelathini mbalimbali yataisikia. Naomba kwa ajili ya kila mtu atakayesikia kanda hii, ambaye hana tumaini hilo la Uzima wa Milele, ambaye hana ubatizo wa Roho Mtakatifu, jalia uje mioyoni mwao kwa utamu. Tujalie hilo, Bwana.

Na hebu mimi, kama sitawaona kamwe katika maisha haya, nitakapovuka na kuingia katika ile nchi, jalia wao naomba wakimbie na kunishika (nami niwashike, na wao, tupaze sauti, "Ndugu wa thamani!" Mmoja kwa mwingine), aseme , "Nilisikia kanda yako ya Waefeso, jinsi ambavyo Mungu alituchagua tangu awali kwa ajili ya Uzima wa Milele, na ilikuwa kwenye hiyo kanda ambapo nilipokea Sauti ya Mungu na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu katika Ufalme wa Mungu." Tujalie hilo, Baba.

Waponye wote walio wagonjwa na wanaoteseka. Jipatie utukufu Mwenyewe kwa kuwa tunakukabidhi yote haya katika jitihada zote katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

Je! Kuna yeyote hapa aliye mgonjwa na anayetaka kuwekewa mikono apate kuombewa? Mwaweza kuinua mikono yenu? Vema. Ungeweza kutembea kwa utulivu, sasa, kuja madhabahuni papa hapa, na kusimama kwa muda kidogo tu, wakati Ndugu Neville akija na ninii yake …

Loo, jambo hili laonekana, kuwaombea wagonjwa, inaonekana tu—inaonekana kama kuja mahali ambapo unajua ulikosimama, hasa. Mungu anajua yote kuhusu hili.

Ninapousikia wimbo huo … Kumbukeni, kama mnaishi nitakapoondoka, uchezeni huu: *Amini Tu*. Kumbukeni, sijafa, sitakuwa mbali sana nanyi kuweza kuusikiliza huo. Siwezi kufa; Yesu alinipa Uzima wa Milele; atanifufua penye ile siku ya mwisho; nitawaona ninyi. Na kama ukiondoka, nitaamini jambo hilo hilo kwa ajili yako. Naamini tutaonana tena.

Nikimwangalia, huyu bibiye wa thamani akiwa amesimama hapa mwenye mvi. Wewe ni Mkristo? Amejazwa na Roho Wake, akimngojea Yeye aje, akiwa amesimama tu hapa nje akingojea mashua ije pale. Amina. Loo, dada …

MESSAGE hub online

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info